Nipashe
Jumamosi Oktoba 21, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581470
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

**Mwinyi:** Tanzania inatekeleza misingi ya haki za binadamu

UKURASA 3



**Korti** yaamuru ubomoaji nyumba kisa deni milioni 3/-


UKURASA 4

**Viwango** duni vinavyosukuma ubinafsishaji katika Bandari

UKURASA 7




UKURASA 11




# Chanzo cha moto Kariakoo chaanikwa

- **Kamera** ya CCTV yakata mzizi wa fitina... *Endelea Ukurasa 2*

## Mzozo Palestina, Israel wawaibua viongozi wa dini

UKURASA 3




## Muhimbili yachanganya miili ya marehemu

UK. 2

**MICHEZO** GAMONDI AANDAA MBINU MPYA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Spika wa Bunge ambaye pia ni Mwenyekiti wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) Kundi la Afrika, Dk. Tulia Ackson, akizungumza na Spika wa Bunge la Angola, Carolina Cerqueira katika Ofisi za Spika huyo, Luanda, Angola jana. Spika Tulia yuko nchini humo kuhudhuria Mkutano wa 147 wa IPU unaotarajiwa kufunguliwa keshokutwa. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Chanzo moto Kariakoo chaanikwa

**Na Beatrice Shayo**

RIPOTI ya Kamati iliyoundwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, kuchunguza moto katika maduka na vibanda Kariakoo jijini Dar es Salaam, imebainisha kwamba chanzo ni hujuma baina ya wafanyabiashara wenyewe.

Hilo limebainika kutokana na kamera za CCTV katika eneo hilo kuonyesha kuwa hakukuwa na hitilafu yoyote ya umeme wala hujuma kutoka nje.

Tukio la moto huo katika maduka hayo lilitokea Oktoba Mosi, mwaka huu, na siku iliyofuata, Chalamila aliunda kamati ndogo ya uchunguzi yenye watu saba ambayo jana ilikabidhi ripoti hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuhusu ripoti hiyo, Chalamila alisema chanzo cha moto huo si ajali bali ni hujuma.

Alisema kamati hiyo ambayo aliipa siku saba kukamilisha hatua za awali za uchunguzi, imebaini moto huo ulianzia katika eneo la Mnadani Kariakoo na haukuwa ajali bali ni hujuma miongoni mwa wafanyabiashara wenyewe.

Chalamila alisema maelezo hayo yamebainika kupitia baadhi ya kamera za CCTV ambazo zilikuwa pembezoni wakati moto huo unaanza taratibu kabla ya kuingia katika majengo mengine.

Alisema awali wafanyabiashara walieleza kuwa moto huo ulisababishwa na jenereta ambalo lilikuwa pembezoni kidogo ya eneo hilo lililotokea ajali ya moto.

"Lakini uchunguzi wetu umebaini kuwa jenereta hilo ni zima na linafanya kazi, halikuungua na wala halikuwa chanzo cha moto huo uliotokea," alisema.

Chalamila alisema kamati hiyo imetoa ushauri na mapendekezo kwa wafanyabiashara wa vyuma chakavu kuwa watafutiwe eneo lingine kwa kuwa imeonyesha kama kutatokea moto, madhara yake yanaweza kuwa makubwa zaidi.

Pia alisema Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, ambayo Kariakoo ni moja ya sehemu zake, imetakiwa kusimamia sheria zinazoelekeza upangaji wa miji na majengo na kutoa mfano wa kuacha njia za wazi za dharura baina ya jengo moja na lingine ili yanapotokea majanga ya aina hiyo, yashughulikiwe kirahisi.

Alisema jambo lingine ni Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ifanye mapitio ya kampuni ya The Kariakoo Auction Mart Limited ili kupata uhalali wa wamiliki.

"Endapo itabaini mpaka sasa hakuna mmiliki halali, eneo hilo litakuwa chini ya udhibiti wa serikali mpaka hapo watakapopata majibu mazuri ya kisheria.

"Ninaomba kusisitiza kwamba pamoja na madhara mengine yaliyojitokeza katika eneo hilo, zaidi ya wafanyabiashara 550 walipata madhara katika maduka yao ambayo hatua za awali zimebainisha walikuwa katika majengo yaliyoshika moto," alisema.

Chalamila alibainisha kwamba uchunguzi huo umehusisha ukaguzi wa eneo la tukio, kufanya mahojiano ya kina na mashuhuda, wamiliki wa majengo na wanaolizunguka.

Pia alisema uchunguzi ulihusisha wafanyabiashara, walinzi wa zamu, maofisa wa zamu waliokuwa wakishiriki kwa pamoja kama sehemu ya lindo la maeneo hayo.

Pamoja na kuzichunguza kamera zote, Chalamila alivielekeza vyombo vyote vinavyoshughulika na masuala ya uvunjifu wa sheria vianze sasa kazi yake ili kuwabaini watu wote ambao walifanya hivyo na kusababisha hasara.

"Nitoe wito kwa wafanyabiashara wote siyo tu maeneo ya Kariakoo, siyo sahihi kufanya vitendo vya hujuma ambavyo vinaweza kusababisha madhara na athari kubwa kwa wananchi ambao hawana hatia.

"Vyombo vinavyoshughulika na masuala hayo sasa vitakabidhiwa nyaraka hizo kwa hatua za awali ili waweze kubaini watu wote ambao wamefanya hujuma hizo kwa maslahi yao ama ya kikundi chao," alisema Chalamila.

Mkuu wa Mkoa alisema watu hao watakapobainika watafikishwa katika vyombo vya dola kwa ajili ya kuchukuliwa hatua.

# Muhimbili yachanganya miili ya marehemu

**Na Waandishi Wetu**

SINTOFAHAMU imeibuka baada ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) kuchanganya miili ya watu waliofariki dunia katika taasisi hiyo.

Mkanganyiko huo umetokea baada ya mwili uliokuwa upelekwe Moshi, mkoani Kilimanjaro kukabidhiwa kwa watu wengine na kuupeleka Songea, mkoani Ruvuma.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano MNH, Aminiel Aligaesha, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo juzi na kueleza kuwa tayari mwili wa Emmanuel Ngowo ambao ulipelekwa Ruvuma umeshakabidhiwa kwa ndugu zake.

Alisema Hospitali ya Muhimbili imelazimika kugharamia kusafirisha mwili huo kutoka Ruvuma hadi Dar es Salaam kwa ndege na uliingia jana na kukabidhiwa kwa ndugu husika.

"Nina sentensi moja tu ndugu waandishi ya kuwaambia. Sina la zaidi ya kuwaambia na kusema hadi sasa tumekamilisha hatua zote na tayari tumeshakabidhi miili yote kwa ndugu wa marehemu ili waende wakaihifadhi.

"Nisikilize vizuri kila familia imeshapatiwa mwili wake. Wa Songea wamepatiwa mwili wao leo (jana) na wanaotakiwa kuzika Kilimanjaro wamechukua mwili wao wamekwenda kuzika," alisema Aligaesha.

Hata hivyo, alipoulizwa sababu za kuchanganywa kwa miili hiyo, alisema: "Ninaomba uchukue hiyo taarifa kwa sasa. Ni vitu vya utawala na vinafanyiwa kazi na utawala."

Baada ya mwili wa Ngowo kufikishwa eneo la msiba, Mazizini, Ukonga Mombasa, ndugu waliupokea kwa mayowe na mmoja wa wanafamilia aliyekataa jina lake lisiandikwe gazetini, alisema wamesikitishwa na kitendo hicho kwa kuwa jana walitakiwa wawe Moshi kwa ajili ya maziko.

Mwili huo ulipelekwa kanisani na baadaye kusafirishwa kwenda Moshi kwa ajili ya maziko.

• **IMEANDALIWA na Pilly Kigome na Beatrice Shayo**

# Waziri awaonya wakiukaji maadili

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, ameiagiza Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB) kuwachukulia hatua wataalamu wanaokiuka maadili ili kuepuka kuichafua kada hiyo.

Kasekenya alisema hayo jana wakati akifungua Mkutano wa Nne wa AQRB kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, unaofanyika jijini Dodoma. Mkutano huo unakwenda sambamba na maonyesho ya kazi za wataalamu hao.

"Kuna wataalamu mmewasajili ila wengine kwa makusudi wanakiuka utaratibu waliowekewa na bodi yenu. Hao msiwavumilie, wafuatilieni na washughulikieni wasije wakawachafulia kazi nzuri mnayoifanya," alisema.

Mhandisi Kasekenya alisema ni vyema wataalamu wasanifu majengo na wakadiriaji majenzi wakaungana ili kutengeneza nguvu ya pamoja ambayo itawasaidia kupata mikataba ya miradi mikubwa ambayo itaisaidia serikali kuokoa gharama za kutafuta wataalamu kutoka nje.

"Tambueni taifa linafahamu mchango wenu na linathamini wataalamu wa ndani ndiyo maana waziri mwenye dhamana ya wizara hii anawashauri muunganishe nguvu ili kupata tenda kubwa hapa nchini. Hii itasaidia kupunguza gharama ya kuwatoa wataalamu kutoka nje ya nchi," alisema. Katika hatua nyingine, Kasekenya alisema wizara itaendelea kutoa ufadhili wa mafunzo kwa vitendo kwa wataalamu wa taaluma za wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi nchini.

Pia alisema bodi itaanzisha mfuko wa maendeleo ya wanafunzi ili kutenga fedha za kusaidia vijana wenye taalamu za ubunifu majengo na wakadiriaji majenzi.

Sambamba na hayo, alizielekeza AQRB, Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) na Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC) kufanya kazi kwa ukaribu na kushirikiana ili kuhakikisha kuwa taifa linafaidika na huduma za kitaalamu zinazotolewa na wataalamu na kampuni zilizosajiliwa na taasisi hizo.

Msajili wa AQRB, Arch. Edwin Nnunduma, alisema bodi ina mpango wa kusajili wataalamu 5,000 kufikia mwaka 2026 katika kada za kati.

Pia alisema ili kuboresha utendaji na ufanisi wa wafanyakazi, bodi inatarajia kuanzisha mfumo wa kielektroniki kwa watumishi wote.

## HABARI KITAIFA




Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Itikadi na Uenezi, Sophia Mjema (katikati), akizungumza baada ya kukagua ujenzi wa jengo la kituo cha afya cha Kassim Majaliwa, Chiola, Nachingwea mkoani Lindi juzi. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Mohamed Moyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi: Tanzania inatekeleza misingi haki za binadamu

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

SERIKALI imesema Tanzania inatekeleza kikamilifu misingi ya haki za binadamu na kulinda vilivyo kwa mujibu wa mikataba ya Kamisheni za Afrika ya Haki za Binadamu na Watu.

Akifungua kikao cha 77 cha kawaida cha Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (ACHPR), Rais wa Zanzibar (SMZ), Dk. Hussein Mwinyi, alisema jitihada mbalimbali zimechukuliwa na serikali katika kulinda haki za binadamu, ikiwemo uhuru wa kutoa maoni. Dk. Mwinyi, alimwakilisha katika mkutano huo, Rais Samia Suluhu Hassan katika mkutano huo ambao kaulimbiu yake ni 'Kuimarisha na Kuendeleza Utamaduni wa Haki za Binadamu kwa Nyakati zijazo'.

"Serikali inatekeleza na kusimamia haki za binadamu kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Katika Katiba yetu, haki za binadamu zimeainishwa kuanzia Ibara ya 12 hadi 24 lakini pia Katiba yetu kuanzia Ibara ya 25 hadi 30 imeainisha wajibu wa kila raia.

"Hapa nchini, jitihada mbalimbali zimechukuliwa na serikali ili kuhakikisha haki za binadamu zinalindwa na kutekelezwa kwa mujibu wa mikataba ambayo Tanzania ni mwanachama kwa kuwa jitihada hizi zimeboresha hali ya upatikanaji wa haki mbalimbali ikiwemo haki ya usawa mbele ya sheria, afya, elimu, maji na mazingira safi, uhuru wa kutoa maoni, uhuru wa kuabudu, ajira, haki ya kumiliki mali na uhuru wa vyombo vya habari," alisema.

Aidha, alisema kutokana na uhuru huo, hivi sasa Tanzania ina vyombo vya habari vingi vikiwemo redio 210, televisheni 56, magazeti 288 pamoja na mitandao mbalimbali ya kijamii. Pia, tumefikia hatua kubwa ya kuimarika kwa uhuru wa kidemokrasia, haki za wanawake, watoto na watu wenye ulemavu kwa kuzingatia usawa wa kijinsia.

"Sote tunafahamu kuwa suala la ulinzi na uhifadhi wa haki za binadamu katika bara la Afrika kwa jumla, bado kwa kiasi fulani linakabiliwa na changamoto. Miongoni mwao ni mapinduzi ya serikali zilizo madarakani, vita vya wenyewe kwa wenyewe, mila na desturi zisizofaa, ukatili wa kijinsia, athari hasi za utandawazi na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu haki zao. Natumia fursa hii kutoa wito kwa nchi na Serikali zote wanachama wa Umoja wa Afrika kuchukua hatua stahiki katika kukabiliana na changamoto hizi," alisema.

Pia alisema katika kuepusha uvunjifu wa haki za binadamu unaotokana na vita, kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania inashiriki katika jeshi la pamoja la kulinda amani mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na kwamba kwa muda mrefu, Tanzania imeshiriki katika ulinzi wa amani katika nchi mbali mbali ikiwemo huko Darfur nchini Sudan na Visiwa vya Comoro.

"Naona fahari kwa Majeshi yetu kwa kazi yao nzuri wanayoifanya. Nitoe wito kwa nchi zetu za Afrika kuendelea kushirikiana katika kuyakabili matukio mbalimbali yanayohitaji msaada wa kibinadamu katika bara letu. Pia niwapongeze makamishina wote wa Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ambao mnashirikiana pamoja katika kuimarisha haki za binadamu na watu katika bara la Afrika.

"Nimejulishwa kuwa katika mkutano huu, yatajadiliwa masuala mbalimbali ikiwemo hali ya haki za binadamu katika bara la Afrika, taarifa za kazi za Makamishna pamoja na taarifa za mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu Afrika. Ni matumaini yangu kuwa taarifa hizi zitatoa tathimini ya hali halisi ya haki za binadamu na kutoa mapendekezo yatakayosaidia kupata mbinu za kukabiliana na changamoto zitakazoainishwa," alisema.

"Nafahamu kuwa kikao hiki kilitanguliwa na majukwaa ya Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu zipatazo 46 na Asasi za Kiraia takribani 210 kutoka Bara la Afrika. Taasisi hizi ni wadau muhimu katika masuala ya ulinzi, utetezi na uhifadhi wa haki za binadamu barani Afrika. Nakupongezeni sana kwa kuona umuhimu wa kuandaa majukwaa ya taasisi na asasi hizo," aliongeza.

Alisema changamoto na majanga mbalimbali ambayo Afrika inapitia, waathirika wake wakubwa ni wanawake na watoto. Kwa kutambua hilo, alisema serikali ya Tanzania imeendelea kuchukua hatua katika kutatua migogoro mbalimbali na kutekeleza kwa vitendo Tamko la Dar es Salaam kuhusu Amani, Usalama, Demokrasia na Maendeleo katika Ukanda wa Maziwa Makuu. Kwa mfano hivi sasa Tanzania inashiriki katika jeshi la Umoja wa Mataifa Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (Stabilization Mission) na Jeshi la Kulinda Amani (MONUSCO).

"Kwa hakika, kaulimbiu ya Siku ya Haki za Binadamu ya Afrika ya mwaka huu, inanishawishi kuwakumbusha ndugu zangu kutoka taasisi za kitaifa za haki za binadamu, AZAKI na wadau wengine wote mliopo hapa kuwa haki za binadamu tunazozitetea ziwe zinaendana na kauli mbiu hii. Kwa ujumla, Bara la Afrika na Tanzania kwa umahususi wake tunaheshimu haki za binadamu kwa kuzingatia utamaduni, maadili na tunu zetu kama Waafrika," alisema.

Pia alisema kauli mbiu hiyo,inashawishi kuwatambua wadau kutoka taasisi za kimataifa na haki za binadamu na Azaki zinazotetea haki za binadamu kuzingatia maadili,utamaduni na tunu zetu za kiafrika.

Mwenyekiti wa ACHPR, Remy Lungu, alisema Tanzania imekuwa kinara wa kudumisha amani ambapo changamoto imekuwa ikitatua yenyewe bila ya kuwapo kikwazo hivyo amezitaka nchi nyingine kuiga mfano huo.

"Hakuna maendeleo bila haki na hatuwezi kuwa na Amani bila maendeleo hivyo haki ni wajibu kwa wanachama,"alisema.

Msajili wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Dk. Robert Eno, akizungumza kwa niaba ya Rais wa Mahakama hiyo, Jiji Iman Abood, alisema tangu kuanzishwa kwa mahakama hiyo miaka 16 iliyopita, imeshatoa uamuzi wa mashauri 100 lakini ni mashauri sita pekee nchi hizo zimefanikiwa kutekeleza.

# Mzozo Palestina, Israel waibua viongozi wa dini

**Na Restuta James**

MZOZO kati ya Palestina na Israel unaoendelea sasa na kusababisha vifo vya watu na uharibifu wa mali, umewaibua viongozi wa dini wakiiomba jumuia ya kimataifa kuingilia kati na kuumaliza.

Viongozi hao ni pamoja na Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania (JMAT) ambayo imesema Umoja wa Mataifa (UN) ufanye kila liwezekanalo kumaliza vita vinavyoendelea katika Ukanda wa Gaza.

Aidha, jumuiya hiyo imetahadharisha kwamba vita vya Gaza si vya kidini na kuwaomba waumini wa dini zote zikiwamo za Kiislam na Kikristo kutogawanyika.

Mwenyekiti Taifa wa JMAT, Sheikh Dk. Alhad Mussa Salum, alitoa tamko hilo jana Dar es Salaam kwa kushirikiana na Kamati ya Mshikamano wa Tanzania na Palestina.

Alisema vita kati ya Israel na Palestina vimekuwa kadhia ya muda mrefu Mashariki ya Kati na dunia imeshuhudia mara kadhaa umwagikaji damu kwa pande zote mbili.

Dk. Salim alisema katika vita vinavyoendelea, kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na sheria za kimataifa katika upande wa Palestina.

Mwenyekiti huyo alisema matukio ya kupiga mabomu nyumba za ibada, hospitali na makazi ya raia yamesababisha kuua na kujeruhi watu wasio na hatia hasa wanawake na watoto.

Alisema wakazi wa Gaza pia, wamekoseshwa huduma muhimu za kijamii kama maji, afya, umeme na elimu ambapo ni kinyume cha haki za binadamu.

"Jambo hili limetuhuzunisha sana kama wapendwa amani duniani. Vita hivi si vya kidini moja kwa moja na visitugawe kati ya Waislamu na Wakristo na watu wa dini nyingine. Wanaouawa pale ni Waislamu, Wakristo, Wayahudi na pengine hata wasiokuwa na dini," alisema.

Kiongozi huyo alisema kinachoendelea Ukanda wa Gaza ni uharibifu ambao ni kitendo ambacho hakikubaliki na watu wastaarabu.

"Tunaziomba na kuzitaka mamlaka husika hasa Umoja wa Mataifa na jumuiya ya kimataifa zihakikishe usitishwaji wa vita hivyo mara moja na kuhakikisha huduma za kibinadamu hasa maji, umeme na dawa zinarejeshwa mara moja. Iangalie kiini cha tatizo hilo ili kupata ufumbuzi wa kudumu," alisema.

Katibu Mkuu wa JMAT, Askofu Dk. Israel Ole-Gabriel Maasa, alitoa rai kwa wapenda amani duniani kupaza sauti za kumaliza mzozo huo ili raia wasio na hatia wasiendelee kupoteza maisha kwa kuwa suala la umwagaji damu halikubaliki.

Vita vinavyoendelea kati ya Israel na Palestina katika ukanda wa Gaza vilianza Oktoba 7, mwaka huu, baada ya kundi la Hamas kuishambulia Israel kwa silaha nzito.

Maelfu ya watu wamepoteza maisha huku wengine wakikosa makazi na huduma muhimu baada ya Israel kulipiza kisasi katika Ukanda wa Gaza.

# PM ashuhudia ukamuaji maziwa kwa roboti

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametembelea shamba la ufugaji wa ng'ombe wa maziwa la Alesandra, Milan nchini Italia, ambalo linaendeshwa kwa kutumia mifumo ya kisasa ya kielektroniki ikiwamo ukamuaji wa maziwa kwa kutumia roboti.

Akiwa katika shamba lenye takribani ng'ombe 500, Majaliwa ameshuhudia mifumo bora ya ufugaji, ulishaji, unyonyeshaji na ukamuaji wa maziwa, ambapo ng'ombe mmoja ana uwezo wa kutoa lita kuanzia 35 hadi 70 kwa siku na kumuwezesha mfugaji kupata tija zaidi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Ofisi ya Waziri Mkuu, Majaliwa alitembelea shamba hilo juzi na kufurahishwa na teknolojia inayotumika katika ufugaji huo.

Majaliwa amekwenda Rome, Italia akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa Jukwaa la Kimataifa la Chakula Duniani lililoanza Oktoba 16 na kumalizika jana.

Viongozi wengine walioambatana naye kutembelea shamba hilo ni pamoja na Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo wa Zanzibar, Shamata Shaame Khamis, ambaye alisema amefurahishwa na misingi bora ya ufugaji.

Alisema utaratibu huo ukitumika Tanzania utaongeza tija katika sekta ya mifugo na kuahidi kwenda kuufanyia kazi.

"Aina ya ufugaji inayotumika kwenye shamba hilo kuanzia hatua uandaaji wa malisho, ukamuaji wa maziwa, usafirishaji na utunzaji wa mifugo niliojifunza shambani hapo nitakwenda kuufanyia kazi lengo ni kuimarisha sekta ya mifugo na kuongeza mapato kwa wafugaji na taifa kwa ujumla," alisema.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akipata maelezo kutoka kwa Alessandra Seresina ambaye ni Mmiliki wa shamba la kisasa la mifugo la Alessandra, kuhusu ufugaji wa kisasa, wakati alipotembelea shamba hilo, Milan, Italia juzi. **PICHA: OWM**

Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, alisema amefurahishwa na uendeshaji katika shamba hilo ambalo wanafanya kilimo mseto kwa kufuga, kulima malisho ya mifugo na kutumia kinyesi cha ng'ombe kuzalisha nishati ambayo wanaitumia kwa shughuli za shambani na ziada kuuza kwenye gridi ya taifa.

Alitaja jambo lingine ni namna ambavyo mifugo yao imewekewa hereni za kielektroniki kwa ajili ya utambuzi ambazo zinaiwezesha nchi kujua idadi ya ng'ombe, maendeleo yake na kutambua magonjwa.

Silinde aliahidi kukutana viongozi wa sekta husika ili kuangalia namna bora ya kuboresha ufugaji nchini.

Mfugali wa ng'ombe kutoka Wami Sokoine, Morogoro, Mainga Ole Kalaita, ambaye alitembelea shamba hilo kwa ajili ya kujifunza ufugaji bora, alisema amepata elimu na atakwenda kuwashauri wafugaji wenzake kubadilika.

Alisema ni lazima wabadilike kuendana na mahitaji ya sasa ya soko ikiwa ni pamoja na kubadili njia za ufugaji na kubainisha kuwa, hakuna haja ya kuwa na mifugo mingi isiyokuwa na tija hivyo ni lazima wafuge kisasa.

Ole Kalaita alisema kuna haja ya wafugaji nchini kukubali mifugo yao iwekewe hereni kwa ajili ya utambuzi wa aina ya uzao wa ng'ombe kwa kuwa, katika masoko ya kimataifa lazima wahoji historia ya mfugo.

Hivyo, aliiomba serikali iendelee kuwaelimisha wafugaji umuhimu wa kuwa na taarifa za mifugo.

Mmiliki wa shamba hilo, Alessandra Soresina, alisema wanatumia teknolojia ya uhimilishaji wa mifugo kwa lengo la kuwa na kosafu za mifugo yao.

Alisema teknolojia hiyo inawasaidia kuwa na uhakika na mwendelezo mzuri wa ng'ombe wanaotoa maziwa kwa wingi.

"Wakati mwingine hutumia akili bandia ili kuweza kubaini mbegu za ng'ombe jike pekee kwa ajili ya uhimilishaji ila njia hii hugharimu fedha nyingi zaidi," alisema."

Alisema ng'ombe wote wanapewa chakula kinachozalishwa shambani hapo kwa kuchanganya mahindi na nyasi zilizohifadhiwa vizuri kwa kutumia teknolojia ya kisasa na mifugo hiyo inapewa chakula mara tatu kwa siku.

"Ratiba hiyo inaweza kubadilika kulingana na msimu. Kwenye shamba hilo hakuna madume na iwapo ikitokea ng'ombe amezaa ndama dume, ndama hao huuzwa," alibainisha.

Soresina alisema ng'ombe wao wamevalishwa hereni ikiwa ni utambulisho rasmi unaohusisha aina, uzao, asili, utambuzi wa mmiliki na kuwezesha ufuatiliaji wa maendeleo yake ikiwamo kutambua magonjwa, uwezo wa kutoa maziwa pamoja na kujua kama anakula vizuri.

# Mahakama yaamuru nyumba kubomolewa kisa deni mil. 3/-

**Na Said Sindo,** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Geita imeamuru kubomolewa kwa nyumba ya Rajabu Mukoko, maarufu Osama, na mali zake kupigwa mnada kufidia Sh. milioni tatu, baada ya kushindwa katika shauri la kujimilikisha na kuuza ardhi ya Hidaya Seleman Issa (68), kinyume cha sheria.

Mukoko aliuziwa eneo hilo na aliyekuwa mume wa Hidaya, Twalib Amri, waliyetengana naye mwaka 2015 kisha mama huyo kuanza kupigwa na kuzuiwa kufika katika eneo hilo na aliyekuwa mume wake.

Mgogoro huo umedumu kwa miaka minane tangu mwezi Juni, 2016 huku mdaiwa namba moja akiwa Twalib Amri (mume wa zamani wa Hidaya) na Rajabu Mukoko (aliyeuziwa eneo hilo) kushindwa kesi hiyo.

Oktoba 17, mwaka huu, mahakama hiyo iliamuru rasmi nyumba hiyo kuvunjwa na vitu kuuzwa ili kumlipa fidia ya Sh. milioni tatu mama huyo.

Akizungumza wakati wa ubomoaji wa nyumba hiyo, Hidaya alieleza kuridhishwa na uamuzi wa mahakama na kusema kesi hiyo alishinda muda mrefu ilikuwa ikisubiriwa amri hiyo.

"Tayari ubomoaji umekamilika nimepatiwa eneo langu pamoja na mali walizonazo ziuzwe kwa ajili ya kulipwa fidia yangu ya Sh. milioni tatu kwa mujibu wa mahakama," alisema Hidaya.

Tabu Masoud ambaye ni muuzaji wa kwanza wa eneo hilo kwa Hidaya, alisema baada ya mama huyo kuondoka, alishangaa kuona eneo hilo linauzwa kwa mtu mwingine lakini hakuhoji kutokana na wawili hao kuwa na uhusiano awali, hivyo alijua kuwa kuna maelewano baina yao.

"Baadaye Hidaya akaja kunitaarifu kuwa ameambiwa eneo lake limeuzwa na mimi nikamwambia niliona lakini nifikiri wamekubaliana. Nimefurahi kuona kapata tena haki yake baada ya kuitafuta kwa muda mrefu," alisema.

Mke wa Rajabu Mukoko (mdaiwa namba moja), Zena Rajabu, alieleza kushtushwa na ubomoaji huo kwa kuwa awali alipopokea barua ya kutakiwa kufanya hivyo lakini alipomkabidhi mume wake, alidai anakwenda kuzungumza naye wayamalize.

"Mimi nilijua yamekwisha cha kushangaza leo hii naona wanakuja kubomoa. Sijajiandaa kwa lolote, baadhi ya vitu nimefanikiwa kutoa lakini vingine vimebaki ndani," alisema.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Magogo, Juma Ramadhan, alisema baada ya kupokea barua ya mahakama alitoa ruhusa kuendelea na majukumu yao ya ubomoaji licha ya kuwapo kwa ukinzani kutoka kwa waliokuwa wamiliki wa nyumba hiyo.

# Wanafunzi 56,132 vyuo vikuu wapata mikopo ya bil. 160/

**Na Beatrice Shayo**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imetangaza awamu ya kwanza ya wanafunzi 56,132 wa shahada ya kwanza waliopangiwa mikopo yenye thamani ya Sh bilioni 159.7 kwa mwaka wa masomo 2023/24 unaoanza wiki ijayo.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, alisema kati ya wanafunzi hao, wa kiume ni 32,264 sawa na asilimia 57 na wa kike ni 23,868 sawa na asilimia 43.

"Kuanzia leo (jana), wanafunzi hao wanaweza kuona tarifa za mikopo waliyopangiwa katika akaunti walizotumia kuomba mkopo. Akaunti hizo zinaitwa SIPA (Student's Individual Permanent Account) ambazo walitumia kuomba mkopo na ndiyo sehemu muhimu ya kupata taarifa kuhusu ombi la mkopo kwa mwombaji mkopo yeyote," alisema Badru.

Badru pia alisema kuhusu utaratibu wa kupokea fedha hizo maafisa wa HESLB watakuwa katika taasisi za elimu yaj uu nchini kuanzia Jumatatu ijayo ili kuratibu usajili wa wanafunzi hao katika mfumo wa malipo.

"Kwa wanafunzi wapya, kama walivyoshauriwa wakati wa kuomba mkopo, wafike vyuoni wakiwa na namba za akaunti zao za benki, namba zao za simu zinazopatikana na watasajiliwa katika mfumo wetu wa malipo wa DiDiS (Digital Disbursement Solution) baada ya kusajiliwa na chuo," alisema Badru.

Pia alisema awamu ya pili ya utioaji mikopo itatolewa kabla ya Oktoba 27, mwaka huu, baada ya kukamilishwa uchambuzi wa maombi unaoendelea na kuwasisitiza waombaji mikopo kutembelea akaunti zao za SIPA kupata taarifa kuhusu maombi yao.

"Orodha hii ya kwanza inajumuisha wanafunzi wenye sifa zikiwamo kuwa wahitaji, wameomba kwa usahihi na wamekamilisha taratibu za udahili wa chuo kimoja. Tunakamilisha uchambuzi wa maombi mengine na tutatoa orodha ya awamu ya pili kabla ya Oktoba 27, 2023," alisema Badru.

Aidha, Badru alisema serikali imetenga Sh. Bilioni 731 kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi 220,376, kati yao, wanafunzi 75,000 watakuwa wanufaika wa mwaka wa kwanza wa shahada ya kwanza na wanafunzi 145,376 wanaoendelea na masomo baada ya kufaulu mitihani yao ya mwaka.

Kuhusu mikopo kwa wanafunzi wa stashahada ambayo inaanza kutolewa katika mwaka huu wa masomo, Badru alisema maombi yanaendelea kupokelewa kwa njia ya mtandao na dirisha litafungwa Oktoba 22, 2023.

Aidha, maombi kwa ajili ya fursa za 'Samia Scholarships' kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu katika tahasusi za sayansi na hisabati yanaendelea kupokelewa hadi Oktoba 22, mwaka huu.

"HESLB inawasihi waombaji wa mikopo wa Shahada ya kwanza, Stashahada na wanufaika wa 'Samia Scholarship' kwa mwaka huu 2023/24 kuwa watulivu wakati taratibu za uchambuzi na upangaji wa mikopo na ufadhili kwa wanafunzi wenye sifa ukiendelea,"alisema.

# Wavunjiwa nyumba madai kuishi hifadhini

**Alphonce Kabilondo, aliyekuwa** KIGOMA

WAKAZI wa Kitongoji cha Katoto B, Kata ya Kagerankanda, Kasulu mkoani Kigoma, wamelalamikia kitendo cha kuvunjiwa nyumba zao, kuchomwa moto na kuamuriwa kuondoka kwa madai ya kuishi eneo la hifadhi.

Wakizungumza na gazeti hili, baadhi ya wananchi walisema tukio hilo lilitokea Oktoba 3, mwaka huu, mchana baada ya magari sita yasiyo na namba za usajili yakiwa na askari wa maliasili kufika hapo na kuanza kubomoa nyumba zao.

Kwa mujibu wa wananchi hao, askari hao walikuwa wameambatana na polisi na kwa pamoja walibomoa nyumba zao na kuzichoma moto, hatimaye kuwataka kuondoka mara moja kwenye eneo hilo.

Mkazi wa Kitongoji hicho, Emanuel Sanagula, alisema siku ya tukio akiwa umbali kidogo kutoka nyumbani kwake, ghafla aliona moshi ukifuka juu na kushuhudia nyumba zikibolewa na kuteketea kwa moto ndipo alipoamua kukimbia kujiokoa.

Alisema kitendo hicho kimesababisha wamepoteze vyakula na mavazi na sasa hawana pa kwenda na kuiomba serikali kuwasaidia.

"Tumeishi pale toka kipindi cha operesheni ya vijiji. Nimeishi katika kitongoji hiki kwa zaidi ya miaka 10 leo tunaamriwa kuondoka na tunachomewa vyakula nakubolewa nyumba zetu, "alisema Sanagula.

Alisema hajawahi kusikia kwenye kitongoji hicho kama kuna kitalu bali anajua mipaka ya kitalu hicho ipo Mto mabele na makombe.

Msomi Sayi, mkazi mwingine, alisema chokocho za kuondolewa zilianza mwezi huu na kwamba, hafahamu kama uongozi wa mkoa unatambua kinachoendelea katika kitongoji hicho. "Tunamwomba Rais Samia Suluhu Hassan, atuangalie kwa jicho la huruma, atusaidie tuishi kwa amani. Tuna zaidi ya wiki mbili tunaishi kama wakimbizi," alisema.

Felista Samueli na Lea Boniphace walisema wameishi eneo hilo kwa muda mrefu na viongozi wakifika hapo na kuwafariji kuwa hatabughudhiwa.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Tawi la Katoto B, Kelelesi Babakelelesi, alisema viongozi wa chama mkoa walishafika kwenye kitongoji hicho na kufungua tawi la chama.

"Leo wananchi wanahangaika nyumba zao zimebolewa na kuchomwa moto, pia vyakula vyao vimeteketezwa kwa moto,"alisema mwenyekiti huyo.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Kagera, Nkanda Nyandura alikiri kuwa kitongoji hicho kimekumbwa na operesheni hiyo lakini hana takwimu sahihi ya kaya zilizobolewa na kuchomwa na moto nyumba zao.

Alisema kitongoji hicho kipo katika wilaya ya mbili za Kasulu na Uvinza.

"Chanzo ni mgogoro wa mipaka kati ya wananchi na kitalu. mgogoro huu haukuanza leo ni toka mwaka 2006 mwekezaji wa kitalu alipopatikana, lakini nimeshafuatilia jambo hili mpaka Wizara ya Maliasili na Utalii lakini hakuna suluhu, "alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Kasulu, Issack Mwakisu, alipotafutwa na Nipashe kwa njia ya simu, simu yake ilikuwa ikiita bila kupokelewa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, Kamishna Msaidizi (ACPO Filemon Mkungu, alisema jeshi hilo linafanya operesheni ya kuwaondoa wananchi wote waliovamia katika Pori Tengefu la Makere na kukanusha kufanya operesheni katika kitongoji hicho.

"Jeshi la Polisi linafanya operesheni ya kuwaondoa waliovamia katika pori tengefu, nitumie fursa hii kuwataka wananchi kufuata sheria za nchini, kumiliki ardhi kunataratibu zake na watambue kuwa, ardhi ni mali ya serikali," alisema Kamanda Mkungu.

## Waziri aonya uuzaji holela wa mashamba

**Na Hassan Mabuye,** SIMANJIRO

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Pinda, amepiga marufuku wenyeviti wa vijiji kuuza viwanja na mashamba kwa kuwa husababisha migogoro ya ardhi isiyo na tija.

Aidha, amemwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, kumsimamisha Mwenyekiti wa Kijiji cha Gitu, Kilindi mkoani Tanga, kwa kuwa ndiye chanzo kikubwa cha migogoro ya ardhi ya eneo hilo.

Pinda alisema mwenyekiti huyo amekuwa akiuza ardhi bila kufuata taratibu za mipango ya matumizi ya ardhi.

Akiwa ziarani katika kijiji cha Kitwai B wilayani hapa, mkoani Manyara, baada ya kukutana na wananchi wa maeneo hayo wenye mgogoro wa mpaka na wilaya ya Kilindi, alisema hakuna mgogoro wowote wa mipaka bali tatizo ni baadhi ya viongozi hususan wenyeviti wa vijiji, kuuza maeneo kwa watu wanaowajua wao.

"Kuanzia leo ni marufuku uuzaji wa maeneo chini ya mamlaka ya wenyeviti wa vijiji sababu ndiyo chanzo kikubwa cha migogoro," alisema.

Pinda pia aliagiza kuondolewa Mpima Ardhi Msaidizi wa Mji wa Mererani, Francis Sulle, kwa kitendo chake cha kuwasumbua wananchi na kukaidi maelekezo ya viongozi wa serikali katika kusimamia masuala ya upimaji na umilikishaji wa ardhi.

"Yule Ofisa Ardhi wa Mererani anasumbua wananchi. Huyu ninaondoka naye kwenda naye Dodoma kwa sababu ameshindwa kufanya kazi yake na amekuwa akikaidi maelekezo mbalimbali anayopewa na viongozi wake wa Wilaya," alisema.

Pinda alisisitiza kuwa utaratibu wa umilikishaji wa ardhi za vijiji unawataja Wakurugenzi wa Halmashauri ambao ndiyo wasimamizi wa utaratibu wa umilikishaji wa ardhi za vijiji na siyo wenyeviti wa vijiji, japo ardhi hiyo inamilikiwa na kijiji.

Alisema hakuna mgogoro wowote wa mpaka baina ya Wilaya za Simanjiro na Kilindi bali kilichotokea ni baadhi ya viongozi wa vijiji kuuza maeneo kiholela yaliyowekewa mipango ya matumizi ya ardhi.



Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhandisi Cyprian Luhemeja (katikati), akifurahia jambo baada ya kufungua Baraza la Wafanyakazi la Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), mjini Morogoro juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Serikali kufanya utafiti maeneo yenye madini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeweka mkakati wa kufanya utafiti wa kijiolojia kubaini maeneo yote yenye madini ili kuondokana na uchimbaji wa kubahatisha.

Waziri wa Madini, Antony Mvunde, aliyasema hayo juzi jijini hapa wakati akiwa katika kikao cha pamoja kati yake na Chama cha Madalali wa Madini Tanzania (CHAMMATA).

Alisema uchimbaji wa kubahatisha umekuwa ukichangia kwa kiasi kikubwa wachimbaji kupoteza fedha zao kwa kuwekeza mitaji mikubwa sehemu ambazo hawana uhakika kama madini yapo.

Mavunde alisema katika kuondokana na hilo, serikali ina mkakati wa kupima maeneo yote ili kuwasaidia wachimbaji kuachana na tabia za kuchimba kwa kubahatisha.

"Suluhisho la kuondokana na tatizo hili ni kufanya utafiti wa kijiolojia. Serikali kupitia uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan imepanga kufanya utafiti nchini nzima ili kubaini maeneo yenye madini ili twende kwenye uchimbaji wa kidunia.

"Leo hii mchimbaji akisikia sehemu kuna madini anakwenda kumbe mwamba wenyewe una urefu wa meza, mtu anawekeza fedha nyingi au (kuchukua) mikopo benki na baada ya muda eneo husika kunakuwa hakuna kitu na yanaanza maneno kuwa biashara ya madini ina majini," alisema Mavunde.

Kupitia mkakati huo, alisema serikali imepanga hadi ifikapo mwaka 2030, maeneo yote yenye madini yawe yamepimwa ili kusaidia wachimbaji wadogo kuendelea kushiriki katika kuongeza pato la taifa kupitia sekta hiyo.

Waziri huyo amewataka mabroka kuendelea kuisaidia serikali kukabiliana na tatizo la utoroshaji wa madini ambao umekuwa ukilipotezea taifa kiasi kikubwa cha mapato.

Alisisitiza kuwa yeyote atayebainika kutorosha madini serikali itamfungia leseni zake zote wakati hatua nyingine za mahakamani zikiwa zinaendelea.

"Hivi karibuni, nilikamata mzigo ambao ulikuwa unatoroshwa kwenda nje ya nchi kule Kahama wa fedha zaidi ya Sh. milioni 500. Mhusika nilimfungia leseni zake zote kwa hivyo, nitoe rai kwa watoroshaji wote wa madini kutafuta kazi nyingine ya kufanya,"alionya.

Mwenyekiti wa CHAMMATA, Jeremiah Kituyo, alisema wataendelea kuisaidia serikali kudhibiti tatizo la utoroshaji wa madini kwa kutoa taarifa.

Hata hivyo, alisema pamoja na mafanikio mbalimbali katika sekta ya madini, bado wanakabiliwa na changamoto ikiwamo ukosefu wa kituo cha afya au zahanati katika eneo la uchimbaji wa madini ndani ya ukuta wa Merelani.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## AFL iwe somo kwa klabu zetu za Afrika Mashariki

**JANA** Afrika imeshuhudia uzinduzi wa mashindano mapya ya African Football League ambayo yanafanyika kwa mara ya kwanza na Tanzania kuwa mwenyeji wa uzinduzi.

Viongozi mbalimbali wa Mashirikisho ya soka, watu mashuhuri duniani katika soka walikutana jana jijini Dar es Salaam kushuhudia sherehe za ufunguzi pamoja na mchezo wenyewe wa ufunguzi kati ya wawakilishi wa ukanda wa kisoka wa Afrika Mashariki na Kati, Simba dhidi ya wawakilishi wa Afrika Kaskazini, Al Ahly ya Misri.

Mchezo huu ulichezwa jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na kuhudhuriwa na maelfu ya mashabiki huku mamilioni ya mashabiki wakiufuatilia kupitia televisheni sehemu mbalimbali Afrika na Duniani kwa ujumla.

Simba imekuwa timu pekee katika ukanda huu kushiriki mashindano haya kwa sababu kuu mbili, kwanza ni kutokana na ubora wao katika kipindi cha miaka mitano ya hivi karibuni, lakini pili umaarufu wao Afrika.

Katika kipindi hicho, Simba imefanikiwa kufanya vizuri kwa kushiriki mashindano yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) na kufikia hatua ya robo fainali mara tatu.

Hii inaonyesha kuchaguliwa kwa Simba kushiriki AFL hakukuwa kwa bahati mbaya, kumetokana na ubora wao waliouonyesha kwenye michuano ya CAF kuanzia ile ya Kombe la Shirikisho na Ligi ya Mabingwa.

Kwa mwaka wa kwanza wa mashindano ya AFL tumeshuhudia timu nane tu zikishiriki ambazo zimetoka kwenye kanda zote za soka Afrika ambazo ni mwanachama wa CAF.

Timu hizo nane mbali ya Simba na Al Ahly, pia zipo Esperance de Tunis ya Tunisia, Wydad Casablanca ya Morocco, Mamelodi Sundowns FC ya Afrika Kusini, TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Atletico Petroleos de Luanda ya Angola na Enyimba ya Nigeria. Kimsingi mashindano haya yachukuliwe kama somo kwa klabu zetu za hapa nchini na Afrika Mashariki kwa ujumla kujiimarisha na kuhakikisha wanapopata nafasi ya kushiriki mashindano ya Kimataifa yanayoandaliwa na CAF wanafanya vizuri.

Kufanya vizuri kwa Simba kwenye Ligi ya mabingwa Afrika na kombe la Shirikisho mara kwa mara kumewapa nafasi ya kushiriki michuano hii ya AFL.

Bado klabu zetu kubwa Afrika Mashariki ambazo zinashiriki mara kwa mara michuano ya CAF, Yanga na Azam za hapa nyumbani, Gor Mahia, AFC Leopard za Kenya, APR ya Rwanda, Vipers na URA za Uganda zinaweza zikapata fursa ya kushiriki mashindano haya kwa miaka ijayo kama watahakikisha wanafanya vizuri kwenye mashindao ya CAF pale wanapopata nafasi.

Yanga msimu uliopita walifanya vizuri kwenye kombe la Shirikisho Afrika kwa kufika hatua ya fainali, tunaamini kama wataendelea kufanya vizuri kwenye michuano ya klabu bingwa wanaweza kupata nafasi ya kushiriki michuano hii yenye pesa nyingi.

Klabu zetu lazima zione wivu na kujipanga kuhakikisha wanaweka malengo ya kushiriki mashindano haya ambayo mwakani yanatazamiwa kuwa na idadi kubwa ya washiriki tofauti na mwaka huu wa kwanza.


Inaelezwa kuna uwezekano timu shiriki katika msimu ujao wa mashindano haya zinaweza kufikia 22, hii inamaana CAf wataongeza wigo kwa timu nyingine.

Ushiriki wa Simba mwaka huu ufungue njia kwa timu nyingine kujipanga na kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye michuano ya CAF

Ukanda wa Afrika Kaskazini kwa mwaka huu wa kwanza, umeingiza timu tatu kutokana na ubora wa klabu zao na mafanikio yao, timu hizo ni Al Ahly, Esperance na Wydad Casablanca.

Tunasisitiza, ushiriki wa Simba mwaka huu kwenye AFL ulete chachu na wivu kwa klabu nyingine za ukanda wetu wa Afrika Mashariki na Kati.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

### Muungwana Lazima Nilonge

## Wachezaji wa Kitanzania nao wakapambane nje ya nchi

**NIMEFURAHISHWA** na maneno ya mchezaji wa zamani wa Mtibwa Sugar na Biashara United, Baraka Gamba Majogolo akiwataka wachezaji wa Kitanzania kuacha tabia ya kulialia kutaka kuonewa huruma ili wawekewe kanuni za kuwadhibiti wachezaji wa kigeni kwenye Ligi ya Tanzania, badala yake amewataka kutoka kwenda kucheza soka nje ya nchi na kupambana.

Majogolo, ambaye hajapitia klabu kubwa za Simba, Yanga wala Azam, kwa sasa anaichezea Chippa United ya Afrika Kusini ambayo inashika nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu nchini Afrika Kusini.

Huwezi kuamini, Majogolo amekuwa kipenzi cha mashabiki wa timu hiyo kutokana na aina yake ya uchezaji wa kujitoa na kuipambania timu.

Mchezaji huyo amewataka wachezaji wenzake wa hapa nchini kutobweteka na kukaa nchini, badala yake kutoka nje na kama wakipata nafasi basi wazitumie kweli ili kupata wachezaji wengi watakaokuwa tegemeo kwenye kikosi cha timu ya taifa.

Majogolo ambaye pia ni mchezaji wa Taifa Stars ameanza kujihakikishia nafasi ya kuitwa baada ya kuamua kutoka nchini na kwenda Afrika Kusini kucheza soka la kulipwa.

Anaungana na Novatus Dismas ambaye anacheza soka la kulipwa nchini Ukraine kwenye klabu ya FC Shakhtar Donetsk na kabla ya hapo hapo nchini alizichezea klabu za Azam FC na Biashara United.

Wachezaji hawa ndiyo wanaonekana kufuata nyayo za Mbwana Samatta na Simom Msuva ambao kwa miaka mingi ndio walikuwa wachezaji waliokuwa wanacheza soka la kulipwa nje ya nchi.

Maneno ya Majogolo yanapaswa kuwa chachu kwa wachezaji wa Kitanzania ambao wameng'ang'ania kucheza hapa hapa wakizunguka timu mbalimbali badala ya kutoka kwenda kutafuta malisho nje ya nchi.

Pamoja na kwamba klabu kutoka nje ya nchi zinaweza kuja kusajili wachezaji nchini, lakini hata wachezaji wenyewe wa Kitanzania wanaweza kusaka nafasi za kucheza kwenye klabu mbalimbali nje ya nchi kama ambavyo tunaona Wakongomani, Wanigeria, Wacameroon na hata Waghana wakija nchini kusaka timu za kuchezea na wamekuwa wakizipata na kuzitumia kama njia ya kusonga mbele kwenye mafanikio.

Wachezaji wa Kibongo waache dhana kuwa wanaweza kutengenezewa kanuni ya kuwalinda ili waendelee kuzichezea klabu za hapa nchini, badala yake waangalie mbele.

Kama wachezaji kutoka Zambia, DR Congo, Rwanda, Burundi, Ghana wanakuja Tanzania kucheza soka kwa nini wao wasiende huko?

Majogolo anaingia kwenye orodha ya wachezaji wachache wa Kibongo waliokeka rekodi ya kucheza Ligi Kuu ya Afrika Kusini.

Majuzi tu nimesikia mdau mmoja akidai itengenezwe kanuni ili timu za Tanzania zitumie makipa wa ndani tu na si wa kutoka nje ya nchi.

Ni yale yale tu, huko tumeshatoka, klabu zinatafuta wachezaji bora na si kulazimika kusajili kutoka wapi.

Yaani Yanga iachane na Djigui Diarra kwa sababu kanuni inataka kipa awe Mtanzania, ni kuitakia mema kweli? Hivi unajua kuwa kipa huyo raia wa Mali alikuwa na mchango mkubwa hadi kufika fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika?

Mbona Aishi Manula anadaka Simba ni namba moja bila hata kanuni? Hapa inaonyesha kuwa hakuna timu inayoweza kumuweka kipa mzuri nje eti kwa sababu si Mtanzania. kinaangaliwa kiwango tu.

Kinachotakiwa ni wachezaji wenyewe wa Kitanzania kupambana, kujituma na kuhakikisha wanapangwa na makocha kutokana na viwango vyao na siyo kwa sababu ya kanuni.

Kwa hali ilivyo na kiwango cha soka la Tanzania kinavyopanda kwa sasa ni aibu kwa mchezaji wa Kibongo kupata namba kwenye timu kwa sababu ya kubabana wageni.

Wapangwe kwa sababu wa viwango vyao, na hivyo viwango ndivyo vitakavyowafanya kufanya vizuri hata kama wakipata timu nje ya nchi kama kina Majogolo.

MAKALA

# Viwango duni vinavyosukuma Bandari Dar es Salaam kwenye ubinafsishaji

Na Mwandishi Wetu

MOJA ya nguzo na sifa za kiuchumi nchini ni bandari, baharini zikiwapo za Mtwara, Tanga na Dar es Salaam, chini ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

Bandari ya Dar es Salaam 'kubwa lao' ndio yenye uwezo zaidi, ikimudu kuhudumia kwa sasa shehena hadi tani milioni 25 kwa mwaka.

Hapo inahudumia meli kubwa zinazoitwa 'Kizazi cha Pili', zenye uwezo kubeba hadi makasha (containers) 2,500. Hata hivyo, inatajwa baada ya kukamilika maboresho yanayoendelea, bandari hiyo itamudu hatua ya juu zaidi kuhudumia meli aina ya "Post Panamax" zenye uwezo kubeba makasha 8,000.

Kwa mujibu wa taarifa za TPA, dira iliyoko ni kuhakikisha malengo ya kiutendaji yanafikiwa, kwa kujumuisha na sifa ya ushindani kimataifa, huduma inatolewa kwa muda mfupi, gharama ndogo, makusanyo ya tozo kuongezeka na zao la yote fursa za ajira zinapanuka maradufu.

Hali iliyopo sasa inatajwa kwamba, Bandari ya Dar es Salaam, iko katika kiwango cha utendaji kumudu kutolewa makasha 12 kwa saa moja, kulinganisha na kiwango kinachoshindana sokoni kwa bandari zingine, kuhudumia makasha 40, kiwango cha tija kilichosimamiwa na Mdhibiti wa Shughuli za Usafirishaji Majini (TASAC).

Zao lake, ni kwamba, Bandari ya Dar es Salaam, haishindana kikamilifu katika soko la Mashariki, Kati na Kusini mwa bara la Afrika.

Changamoto hizo zinatajwa kuifanya bandari hiyo kutumia huduma mbadala wa mifumo iitwayo kama 'ICD' na 'CFS', kutunza na kuhudumia shehena inapoachwa bandarini, kunapotokea mrundikano wa shehena, hata kushindwa kupokea meli zinazoendelea kuongezeka.

Ugumu mwingine unaonekana hapo ni kwenye meli za mafuta kusubiri siku nne hadi tano kushusha shehena, kwa kukosekana miundombinu ya kutosha kuyahifadhi nchini.

Vilevile, inatajwa gharama za kusafirisha shehena kwa meli kuja Bandari ya Dar es Salaam, iko juu maradufu, ikitajwa ni Dola za Marekani 1,000 kwa kasha moja, ikilinganisha na gharama ndogo za bandari shindani.

"Hii inatokana na ukweli kwamba, kwa sasa kuna meli chache sana zenye kufanya safari za moja kwa moja kuja Bandari ya Dar es Salaam," inasema taarifa ya ufafanuzi kutoka TPA.

Hiyo inatajwa kuendana na kukosekana huduma ya kupakua mizigo kwa mkanda au 'conveyer belt' inayopunguza muda wa malori ya kupakia mizigo banadarini na hakuna muunganiko wa moja kwa moja kati ya njia za barabara, reli na meli zinazotoa huduma katika maziwa makuu, kuhakikisha mnyororo wa usafirishaji kuwa rahisi na nafuu kwa bandari nchini.



Huduma zikiendelea bandarini Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA.**

Vilevile kuna malalamiko ya uadilifu katika huduma bandarini, kunyayapaliwa shehena zenye faida kidogo, haki kadhalika umakini kuhakikisha vitu kama dawa za kulevya zinapitishwa.

Hadi sasa, mwelekeo uliopo ni serikali imeshachukua hatua kuiwezesha Bandari ya Dar es Salaam na sekta hiyo kwa upana, kuongeza kasi na ufanisi wa huduma zake kutoa mizigo kufikia mageuzi makubwa ya ufanisi.

Ili kupata mwelekeo wa tija hiyo, ndio dhana ya serikali ya ubinafsishaji bandari nchini inachukua nafasi sasa.

### UKUSANYAJI MAPATO ULIVYO

Katika kipindi cha miaka sita kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2021/2022, TPA haikuweza kukusanya mapato ya malengo tarajiwa.

Mapato kwa Kipindi cha Mwaka 2015/16 hadi 2021/22. Mapato kwa Shilingi Bilioni. Kiwango kilichopatikana kwenye mabano kiwango cha mabilioni.

1. Mwaka 2015/16; Sh. bilioni 624 (Sh. bn 672)
2. Mwaka 2016/17; Sh. bilioni 1,016 (Sh. bn.742)
3. Mwaka 2017/18; Sh. bilioni 1,019 (Sh. bn 817) 4. Mwaka 2018/19; Sh. bilioni,1,013 (Sh. bn.939)
5. Mwaka 2019/20; Sh. bilioni 1,040 (Sh. bilioni 900)
6. Mwaka 2020/21; Sh. bilioni 1,160 (Sh. bilioni 910)
7. Mwaka 2021/22; Sh. bilioni 1123 (Sh. bilioni 1,054)

### KWANINI SEKTA BINAFSI?

Jicho kuu la kuikaribisha sekta binafsi, yenye tija na weledi katika shughuli za kibandari, ili wakati wa kuihudumia iendane na maboresho ya kina kimasoko, kiufundi na kiuwekezaji kufikia ubora unaotakiwa unaomudu ushindani wa bandari kimataifa.

Mtazamo wa kwanza tarijiwa wa serikali, ni kwamba itachangia kuleta mageuzi ya utendaji kukomboa muda wa kuhudumia meli kusubiri kutoka siku tano hadi saa 24, muda wa kupakua makasha, kutoka wastani wa siku 4.5 hadi siku mbili.

Vilevile, mkakati wa serikali ni kupunguza gharama za usafirishaji kwa kuwapo mnyororo wa usafirishaji, utakaoletwa na sekta binafsi, ukipunguza gharama za kusafirisha kasha kutoka Dar es Salaam hadi masoko jirani nchi kama Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), mjini Lubumbashi, Zambia na Malawi.

Ni mkakati unaolenga kushushiwa bei kwa wastani asilimia 50 ya gharama za kusafirisha kasha kwa njia ya meli, kiwango kitakacho shindanishwa dhidi ya bandari jirani kama Mombasa, Kenya.

Hapo inatajwa tena haja ya kuwapo kile wataalamu wa uchumi wanakiita 'multiplier effect; kwamba jambo moja huzua lingine, mapato ya serikali yataongezeka kutokana na ongezeko la shehena na shughuli za kibandari nchini.

Sambamba na hilo, inatajwa uwekezaji wa mifumo ya kielektroniki unaofanywa na sekta binafsi, utawezesha kunasa taarifa sahihi za mizigo kuanzia ilipopakiwa hadi itakaposhushwa, zao lake ni kudhibiti ukwepaji kodi uliopo mahali hapo.

Inakadiriwa mianya inayotumika kukwepa kodi, hususani kutoa taarifa zisizo sahihi za mizigo itazibwa kwa kutumia mifumo ya kielektroniki, inapopakiwa hadi kushushwa.

Ni dira ya mpango mkakati kuifikisha kuwa bandari yenye ushindani wa hali ya juu na inayozalisha ajira maradufu kitaifa, ikiwa zao la ushirikishwaji sekta binafsi kiuchumi na kibiashara.

Lengo kuu hadi sasa imewekwa katika mwaka wa fedha 2021/22, hadi ajira 71,907 mwaka 2032/33 sawa na ongezeko la asilimia 148, baada ya kufanyika ubinafsishaji.

### CHANGAMOTO BANDARI DAR

-Kutokuwapo gati za kutosha; ina jumla ya gati 12 kuhudumia shehena magari, mzigo mchanganyiko, gati mbili za mafuta na kituo kimoja baharini cha kupokea shehena ya mafuta.

Gati hizo 12 zilizopo zina uwezo wa kupokea hadi meli 10 kwa wakati mmoja, nyingine 16 zikisubiri kwenye nanga, kusababisha msongamano na tozo ya adhabu ya meli kuchelewa gatini.

-Uhaba Mitambo ya Kisasa, ikilinganishwa na bandari nyingine.

-Kukosekana Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ya kisasa kuratibu shughuli na huduma bandarini, meli, shehena na utawala.

-Kutofikia viwango vya kimataifa vya huduma za bandari. Meli hukaa gatini na kusubiri kutumia siku 9.5, wakatio viwango ni kimataifa ni siku nne. Pia muda wa mzigo kukaa bandarini kimataifa ni siku mbili, Dar es Salaam, hukaa siku 7.8.

-Kutokuwapo maeneo ya kutosha ndani na nje ya bandari ya kuhifadhi shehena na maegesho ya meli. Kwa sasa, wastani wa meli kwa siku zinazosubiri kuingia bandarini kuhudumiwa ni 16 na wastani wa gati kuhudumia ni meli meli 10 kwa wakati mmoja.

**-Makala hii imeandaliwa kwa mujibu wa taarifa mbalimbali za Mamlaka ya Bandari Tanzania na Serikali.**

HABARI KITAIFA



Rais wa Shirikisho la Sanaa za ufundi Tanzania (TAFCA), Adrian Nyangamalle (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, wakati akitangaza kuanza kwa maonyesho ya kazi za ufundi samani mwezi huu. Katikati ni Mkurugenzi wa Kampuni iliyoandaa maonyesho hayo ya Art & Home, Ameniel Lukumay na Meneja Bidhaa wa kampuni hiyo, Neema Fredrick. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Rais Samia aendeleza mazuri yaliyoanzishwa na Nyerere NIT

**Na Mwandishi Wetu**

OKTOBA 14 ni siku maalum iliyotengwa kwa ajili ya kumbukumbu ya mwasisi wa taifa la Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere na taasisi mbalimbali zimekuwa zikimkumbuka kwa namna ya kipekee kutokana na mchango wake kwa nchi.

Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) siku hiyo hakikuwa nyuma katika kuadhimisha siku hiyo kutokana na ukweli kwamba alitoa wazo la kuanzishwa kwake na hatimaye mpaka sasa kimetoa wataalamu ambao wametoa mchango mkubwa katika sekta ya uchukuzi. Dira ya Nyerere kwa NIT ilikuwa kuona taasisi hiyo inakidhi mahitaji ya rasilimali watu katika sekta hiyo.

Mkuu wa NIT, Prof. Zacharia Mganilwa, alisema baada ya maono hayo ya Mwalimu Nyerere, chuo hicho kilianzishwa mwaka 1975 kama kitengo cha mafunzo cha lililokuwa Shirika la Taifa la Usafirishaji (NTC).

"Taasisi ilipewa jukumu la kuimarisha uwezo wa kuzalisha rasilimali watu ili kuhudumia sekta ya uchukuzi na kuzalisha maofisa usafirishaji wasimamizi wa ngazi ya kati wa kampuni tanzu za NTC. Kampuni tanzu hizo zilikuwa KAMATA (kampuni ya Mabasi Tanzania), Shirika la Usafiri Dar-as-Salaam (UDA) na Kampuni za Usafiri za Mikoa (RETCO)," alisema.

Alisema baada ya kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) mwaka 1977, Kenya ilibaki na Chuo cha Bandari kilichoko Mombasa na Chuo cha Reli cha Nairobi na Uganda ikawa na Chuo cha Anga huku Tanzania ikiwa na Chuo cha Takwimu pekee. Wakati huo pia, Tanzania ilikuwa katika uchumi wa viwanda na Mwalimu Nyerere alitaka kuona NIT inazalisha wataalamu wengi ili kusimamia sekta ya uchukuzi iliyokuwa na mahitaji mengi zaidi.

Prof. Mganilwa alibainisha kuwa mwaka 1982 ilibainika kuwa kuna haja ya kuwa na chuo ambacho kitatoa mafunzo kwenye nyanja zote za usafiri na usafirisaji zikiwamo anga, barabara, reli na maji.

"Kutokana na mahitaji hayo, NIT ilianzishwa upya kupitia Sheria Na. 24 ya mwaka 1982 kama taasisi inayojitegemea ya elimu ya juu iliyokuwa chini ya Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi. Sheria hiyo ilianza kutumika Julai Mosi, 1983 baada ya tangazo kwenye Gazeti la Serikali Na. 91.

Lakini hivi sasa, taasisi iko chini ya Wizara ya Uchukuzi ikisimamiwa kisheria na Baraza la Uongozi wa Chuo," alisema.

Anasema serikali iliyoko madarakani chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, imeendelea kuisaidia NIT katika kuhakikisha mipango yote iliyoasisiwa na Mwalimu Nyerere kwa chuo inafanikiwa kama ilivyopangwa.

Serikali imewekeza kwa kiasi kikubwa katika kuboresha sekta ya uchukuzi ikiwa ni pamoja na kuwekeza kwenye ujenzi wa barabara, reli ya kisasa (SGR), ujenzi wa meli na ununuzi wa ndege katika mkakati wa kulifufua shirika la ndege la taifa (ATCL).

"Maendeleo yaliyofanywa chini ya serikali ya awamu ya sita, yanaisukuma taasisi yetu kuongeza idadi ya wanafunzi na kuanzisha programu mpya kama vile mafunzo ya uhandisi wa usafiri wa anga, mafunzo ya marubani," alisema.

Mganilwa alisisitiza kuwa serikali imeendelea kukiwezesha chuo ili kutimiza wajibu wake wa kuandaa wataalam katika sekta ya uchukuzi kwa maendeleo ya taifa.

Pia alisema chuo kitaendelea kupanua wigo wa mafunzo kulingana na mahitaji katika sekta ya ucuhukzi katika usafiri wa barabara, reli, anga na majini.

**ILANI YA CCM**

Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCMO ya mwaka 2020- 2025 inaielekeza serikali kuendelea kukisaidia chuo hicho ili kutoa wataalam wengi zaidi katika sekta ya uchukuzi.

Katika kutekeleza majukumu yake, NIT kwa msaada wa serikali, imeboresha miundombinu ya kufundishia na Prof. Mganilwa anaishukuru serikali kwa kuendelea kuweka bajeti inayoiwezesha NIT kuboresha mazingira ya kufundishia.

Katika kuiunga mkono NIT, serikali imekipatia Chuo cha Taifa cha Usafirishaji ndege mbili za injini moja, Cessna Skyhawk 172 kwa ajili ya kuendesha mafunzo ya anga hususani kozi za urubani.

Chuo hicho kilipewa ithibati kamili na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET) kutoa mafunzo ya elimu ya juu yanayozingatia Umahiri (CBET) katika ngazi za cheti, diploma na Shahada (NTA ngazi ya nne hadi ya nane).

Aidha, kimeidhinishwa na taasisi ya Chartered ya Logistic na Taransport (CILT International) kufundisha programu za vyeti za kimataifa, stashahada ya kawaida na stashahada ya juu kwenye logistiki na usafirishaji.

Chuo pia kinashirikiana na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) na Taasisi ya Kimataifa ya Menejimenti ya Ununuzi na Ugavi (IPSCMC) kutoa shahada ya uzamili katika menejimenti ya logistics na usafiri na stashahada ya uzamili ya usimamizi wa ununuzi na ugavi.

Mbali na kozi hizo, pia imaendesha programu za usimamiaiz wa logistiki na usafiri, forosha, uhandisi magari, uongozi wa biashara, teknolojia ya Habari na mawasiliano, usafiri wa anga na menejimenti ya rasilimali watu.

# Waziri ahamasisha Watanzania kuchangamkia fursa soko AGOA

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, amesema biashara baina ya Tanzania na Marekani bado ni ndogo, hivyo kuwataka Watanzania kuchangamkia fursa ya kuuza bidhaa Marekani kupitia soko la AGOA.

Aliyasema hayo juzi wakati wa utiaji saini makubaliano ya majadiliano ya kibiashara kati ya Marekani na Tanzania, hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Dk. Kijaji alitoa mfano kuwa mwaka 2022 mauzo ya Tanzania kwenda Marekani yalikuwa na thamani ya Dola Marekani milioni 74.5 na ununuzi ulikuwa na thamani ya Dola za Marekani milioni 93.7.

"Kwa hiyo jitihada zaidi zinahitajika katika kukuza biashara na tunaamini, makubaliano tuliyosaini leo yatasaidia zaidi katika kukuza biashara na Marekani," alisema.

Waziri alitaja maeneo ambayo wamekubaliana kuanza nayo majadiliano kupitia makubaliano hayo kutokana na umuhimu wake kuwa ni, uchumi wa kidigitali, upatikanaji wa masoko, mifumo ya kisheria na mazingira ya biashara, ushirikiano kwenye maonyesho ya biashara.

"Maeneo haya ni ya kuanzia. Maeneo mengine yatakuwa yanaongezwa kadri itakavyoonekana inafaa kwa manufaa ya pande zote mbili. Ninaomba nitoe rai kwa sekta binafsi kutumia fursa hii vizuri kwa kubainisha maeneo ambayo yanawapa changamoto wakati wa kufanya biashara na wenzetu," alisema.

Alisema watakapobainisha changamoto watakaa pamoja na kuongea na Marekani kuona namna ya kutatua masuala hayo, ili biashara iendelee kukua na kuinua vipato vya wananchi na mapato ya serikali.

Waziri Kijaji alimshukuru Waziri wa Biashara wa Marekani, Gina Raimondo, kwa ushirikiano wake katika suala hilo na kuahidi kuendelea kushirikiana naye kuhakikisha kuwa, biashara baina ya nchi hizo inaendelea kukua na kuimarika.

Aliwakaribisha wafanyabiashara kutoka Marekani kuja Tanzania kufanya biashara na kujenga viwanda vya kuzalisha bidhaa ambazo zitauzwa nchini, na kwenye masoko ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na soko la Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA).

Balozi wa Marekani Nchini, Dk. Michael Battle, alisema anafurahishwa na mageuzi makubwa ya kiuchumi yanayofanywa na serikali katika nyanja za kisiasa na kiuchumi.

"Ni imani ya serikali ya Marekani kwamba, ukuaji wa uchumi na utawala bora ni mambo yanayokwenda sanjari. Demokrasia ya kweli inajenga uchumi, na uchumi imara unajenga demokrasia," alisisitiza.

Balozi huyo alisema kupitia makubaliano hayo, wafanyabiashara wa Marekani na Tanzania watakutana mara kwa mara, hali ambayo itaiwezesha sekta binafsi kuchangia katika ukuaji wa uchumi na kuimarisha uhusiano wa kibiashara uliopo baina ya mataifa hayo.



## Mavunde azungumzia kero jimboni kwake

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MBUNGE wa Dodoma Mjini (CCM), Anthony Mavunde ametaja mikakati ya Serikali kutatua kero zinazowakabili wananchi wa Kijiji cha Zepisa Kata ya Hombolo Makulu ikiwamo ya ukosefu wa maji na kushindwa kushiriki katika shughuli za maendeleo.

Akizungumza na Nipashe, Mavunde ambaye pia ni Waziri wa Madini, alisema amekuwa mstari wa mbele kutatua kero hizo na zipo hatua ambazo zimeendelea kuchukuliwa, ikiwa ni pamoja na Serikali kuwa katika hatua za mwisho kumpata mkandarasi wa kusambaza maji kwenye kijiji hicho.

Alisema alipochaguliwa alikuta kata hiyo ina tatizo kubwa la upatikanaji wa maji na kuanza kuchimba visima kwenye eneo hilo na Kijiji cha Zepisa, Serikali kupitia fedha za UVIKO-19 ilielekeza kuchimbwa kisima cha maji chenye uwezo wa kuzalisha lita 22,000 kwa saa.

"Changamoto ilikuwa imebaki ni namna ya kuwafikia wananchi yaani usambazaji na kwa sasa tangazo la kumpata mkandarasi limewasilishwa mfumo wa ununuzi wa umma... niwape pole wananchi wangu kwa sababu hii ni changamoto nitahakikisha tunaitatua kwa wakati, " alisema.

Kuhusu ujenzi wa zahanati ya Zepisa, alisema ujenzi wake ambao ulisimama kwa takribani miaka 17 umekamilika na inatarajiwa kufunguliwa hivi karibuni.

"Changamoto ya umeme tumepata mradi mkubwa wa usambazaji umeme ambapo kwa Dodoma tulikuwa tumebakiza maeneo machache ambayo hayajafikiwa, nilishamuelekeza Diwani kukutana na Meneja wa Tanesco na mkandarasi anatarajiwa kufikisha umeme kwenye Zahanati hiyo na shule ya sekondari mpya tuliyojenga," alisema.

"Suala la barabara wamekuwa na changamoto sana njia ya kupitia Nzasa tumeifungua hivi karibuni na barabara ya Zepisa hadi Hombolo Makulu mkandarasi yupo hatua za mwisho kupatikana na zabuni itafunguliwa Oktoba 30, 2023 na wiki iliyopita alikwenda Meneja wa Tarura na nilielekeza kabla ya mvua wahakikishe eneo hilo linarekebishwa,"alisema.

Alisema jimbo hilo lina mitaa 222 na ameendelea kufanya jitihada za kushughulikia kero zinazowakabili wananchi wake na kuwatoa hofu kuwa serikali itatatua kero zao.

Juzi, wananchi hao waliiomba Serikali kuwapelekea huduma muhimu za umeme, maji na barabara.

Mkazi wa Kijiji hicho, Elizabent Mathonya, alisema tangu ahamie kijijini hapo mwaka 1972 hapajawahi kuwa na huduma hizo.

# Waziri Jafo ataja fursa vijana kujiajiri

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

VIJANA nchini wametakiwa kutumia fursa zitokanazo na utunzaji wa mazingira na kuokoa viumbe hai ili kujikwamua kiuchumi kupitia miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, alisema hayo jana wakati akifungua mkutano wa vijana zaidi ya 100 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar, wenye lengo la kujadiliana namna bora ya kutumia fursa zinazotokana na utunzaji wa mazingira.

Jafo, alisema kuelekea mkutano wa 28 wa nchi wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28), unaotarajiwa kufanyika Umoja wa Falme za nchi za Kiarabu kuanzia Novemba 30 hadi Desemba 12 mwaka huu vijana wanatakiwa kutumia fursa zitakazojitokeza katika mkutano huo kujikwamua kiuchumi.

"Bado kuna changamoto zinazoikumba sekta ya mazingira kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yamekuwa yakiathiri uhai wa viumbe hai na misitu, hivyo ni vyema kama vijana kutumia fursa za utunzaji wa mazingira kujiingizia vipato vyao," alisema Jafo

Alisema kuna takataka zimekuwa zikibadilishwa kuwa fursa kama magurudumu ya magari kutengeneza meza au viti vinavyoweza kutumika tena, makopo ya plastiki mapambo.

Aliwataka vijana kuiokoa nchi isiingie kwenye jangwa kwa kufanya ubunifu wa bidhaa kama ambavyo Serikali imeweka kipaumbele kwao kusaidia taifa kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Mshauri wa Rais kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, Dk. Richard Muyungi, alisema Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa ni kinara wa kupinga uchafuzi wa mazingira na kutoa baadhi ya maagizo kwa watendaji kutafuta njia bora ya kupambana na hali hiyo.

"Hivyo katika kumuunga mkono ni lazima watendaji kuhakikisha katika shughuli tunazofanya zizingatie usalama wa mazingira ikiwa ni pamoja na kupanda miti, kulinda vyanzo vya maji, kuzuia utupaji wa taka hovyo na kusisitiza wananchi kuacha kutupa taka hovyo," alisema



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (kushoto), akikabidhi hati miliki ya kiwanja kwa mkazi wa Nkuhungu, Emanuel Nalogwa ambaye ni mmoja wa wananchi waliohudhuria kliniki ya ardhi iliyoandaliwa kutatua kero za ardhi inayoendelea viwanja vya ofisi ya zamani ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma jana. Wengine ni Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (wa pili kushoto) na Mkurugenzi wa Jiji hilo, John Kayombo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wizara yawalipa wananchi kifuta machozi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WIZARA ya Maliasili na Utalii imetumia Shilingi milioni 40 kuwalipa kifuta machozi wananchi baada ya tembo kuharibu mashamba yao na kusababisha vifo vya watu mkoani hapa.

Aidha, Wizara hiyo inafanya tathmini ya madai ya wananchi 123 yenye thamani ya Shilingi milioni 37 kwa ajili ya kuwalipa fidia kwa kupata madhara ya tembo hao.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Dunstan Kitandula, akizungumza na wananchi juzi kwenye mkutano wa hadhara mjini Singida, alisema wizara inafanya utaratibu wa kuondoa usharoba ambao ulivamiwa na wakulima wa korosho na kusababisha tembo kukosa mapito.

Akizungumzia maendeleo ya sekta ya utalii, alisema idadi ya watalii kutoka nje ya nchi imeongezeka kutoka 600,000 mwaka jana hadi kufikia 2,200,000 juni mwaka huu.

Kitandula alisema watalii wa ndani wameongezeka kutoka 750,000 hadi kufikia 2,600,000 kwa kipindi hicho, ongezeko hilo limetokana na uhamasishaji uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kupitia filamu ya Royal Tour.

"Sekta ya utalii leo hii inachangia mapato ya fedha za nje kwa asilimia 25 na inachangia zaidi ya asilimia 17 ya pato la taifa, haya ni maendeleo makubwa katika sekta ya utalii," alisema.

Kitandula aliongeza kuwa World Tour wamevitambua vivutio vya utalii nchini ambapo hifadhi ya Serengeti imepewa hadhi kuwa kivutio bora kwa ukanda wa Afrika.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni akizungumza katika mkutano huo, alisema zaidi ya askari 17,000 wameajiriwa katika Jeshi la Polisi katika kipindi cha miaka miwili na nusu.

Alisema asilimia 80 ya askari wa jeshi hilo wamepandishwa vyeo na bajeti ya wizara hiyo ikiongezeka katika kipindi hicho kwa zaidi ya asilimia 44.





## Wafanyabiashara wavunjiwa vibanda ufukweni

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

KAMISHENI ya Utalii Zanzibar imeanza operesheni maalumu ya kuwaondoa wafanyabiashara kwa kuvunja vibanda walivyojenga katika fukwe za bahari kwa lengo la kusafisha mazingira.

Operesheni hiyo endelevu imeanza juzi katika Kijiji cha Kendwa na Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Akizungumza na waandishi wa habari, katika eneo la Nungwi, Ofisa Uhusiano wa wa Kamisheni hiyo, Ahlam Othman Abdallah, alisema ni kinyume na taratibu na sheria kufanya ujenzi katika fukwe za Bahari ya Hindi.

Alisema fukwe za Kendwa na Nungwi zimebanwa kwa kujengwa mabanda ya biashara na kugeuka kero kwa watalii.

"Watalii wanahitaji utulivu ili kuenjoy na fukwe zetu mwanana tulizonazo, lakini hali ni tete katika fukwe kumejengwa mabanda ya biashara kama tupo soko la mboga na matunda, " alisema.

Alisema awali walitoa taarifa na kuwapa elimu wafanyabiashara hao kuhama katika maeneo hayo kwa kuwa hayapo kisheria kwa biashara.

Alisema kamisheni kwa kushirikiana na kikosi cha askari utalii wameamua kufanya operesheni katika maeneo hayo kwa kuwaondoa walikaidi amri hiyo na kuchukua bidhaa zao.

Mtaalamu wa Mazingira kutoka Idara ya Mazingira, Bakari Abdallah Bakili, alisema kujenga mabanda katika fukwe hizo kuna athari zake kimazingira ikiwemo kusababisha maji ya bahari kupanda katika makazi ya wananchi.

Alisema Zanzibar ina vivutio vingi vya utalii ikiwemo fukwe hizo na kusifika duniani, hivyo ni lazima zilindwe, zitunzwe na zihifadhiwe.

Alisema sheria ya ardhi inapiga marufuku kufanyika ujenzi zaidi ya mita 30 kutoka katika kingo za maji ya bahari ili kudhibiti mmomonyoko wa fukwe.

Kwa upande wao wafanyabiashara hao walihoji sababu za kutozwa ushuru kwenye mabanda hayo kama sheria hairuhusu.

"Hapa tunalipia Shilingi 200,000 kwa mwezi ada ya kufanya biashara, usafi, ulinzi sasa kama sheria hairuhusu kwa nini walituchukulia fedha zetu," alisema Riziki Juma, mfanyabiashara wa vinyago, shanga na mabazi kwa ajili ya watalii.

Aliitaka Serikali kuwawekea mazingira rafiki ya kufanya biashara zao katika sekta ya utalii ili wajiajiri na kuachana na utegemezi.

# Uhaba wa dola waikumba Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZANZIBAR imekumbwa na uhaba wa dola hali iliyosababisha bei ya bidhaa muhimu kama chakula na mafuta kupanda bei.

Wakizingumza na Nipashe, baadhi ya wafanyabiashara walisema upatikanaji wa dola kutoka benki za biashara umekuwa mgumu ambapo mnunuzi kabla ya kuuziwa hutakiwa kueleza sababu ya matumizi yake.

Aidha, walisema mnunuzi anauziwa si zaidi ya dola 500 kwa siku, hali inayowafanya wafanyabiashara kushindwa kuagiza bidhaa kwa wakati.

Mmoja ya wafanyabiashara hao, Mohammed Ali, alisema anashindwa kuagiza viatu kwa sababu hana fedha na kutosha kutokana na dola kuadimika.

Mfanyabiashara mwingine, Mussa Omar, alisema hajasafiri kwa zaidi kwa mwezi sasa kwa sababu ya ukosefu wa dola.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk Saada Mkuya Salum amethibitisha kuwepo kwa upungufu wa dola visiwani hapa.

"Dola hazijaadimika Zanzibar tu ni Tanzania nzima na baadhi ya nchi duniani, hii inatokana na sera ya Marekani ya kupunguza mzunguko wa dola katika uchumi wake ili kujikwamua na changamoto ya kupanda kwa bei za bidhaa na huduma," alisema.

Hata hivyo, alisema Serikali kupitia Benki Kuu Tanzania (BOT) inaendelea kuchukua hatua ikiwemo kuongeza mzunguko kutoka dola milioni moja hadi kufikia dola milioni mbili kwa siku kupitia soko la kubadilisha fedha.

Alisema licha ya kuongeza mzunguko, kipaumbele kimewekwa kwa waagizaji wa bidhaa za chakula na mafuta huku BOT ikianza utaratibu wa kununua dhahabu na kuiweka dhamana katika masoko ya nje ili kupata dola.

Njia ya kukabiliana na upungufu huo ni kuweka mkazo wa matumizi ya fedha za ndani katika huduma za kawaida ikiwemo malipo ya ada za shule na ya huduma za nyumba.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe, umebaini uagizaji wa bidhaa ulipungua kwa kiwango kikubwa Agosti mwaka huu.

Kwa kipindi hicho, bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 115.7 ziliagizwa ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 162.9 zilizoagizwa Julai ambapo kuna upungufu wa asilimia 29.0 sawa na Shilingi bilioni 47.2.

Kupungua kwa uagizaji bidhaa kulichangiwa zaidi na kushuka kwa Shilingi bilioni 15.3 kwa matumizi ya bidhaa za kati zinazotumiwa na watengenezaji kutoka Shilingi bilioni 52.7 Julai mwaka huu.

Wazalishaji wa Zanzibar kwa kiasi kikubwa wanategemea masoko ya nje kwa usambazaji wa vifaa.

Matumizi ya mafuta ambayo ndiyo kichocheo kikuu cha uagizaji bidhaa, pia yalipungua kutoka Shilingi bilioni 57.7 Julai hadi Shilingi bilioni 52.7 Agosti, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Dk. Ulrick Mumburi, hadi Agosti 2023, BOT ilikuwa na akiba ya dola milioni 5,441 za Marekani ambazo zingetosha kwa miezi 4.9 ya uagizaji bidhaa na huduma nje ya nchi.



Mwanafunzi James Emmanuel wa Shule ya Msingi Rorya ya jijini Mwanza, akipokea cheti cha kuhitimu elimu ya Msingi kutoka kwa mgeni rasmi Mhandisi Nyerere Lucas, katika mahafali yaliyofanyika shuleni hapo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Sheria ya mtoto yatakiwa ibadilishwe'

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Maendeleo ya Ustawi wa Jamii Jinsia Wazee na Watoto imesema wakati umefika wa kuifanyia marekebisho ya sheria ya mtoto ili iendane na mabadiliko yanayoendelea kutokea duaniani.

Sheria hiyo namba 6 ya mwaka 2011 inatakiwa kubadilishwa na kuja na sheria ambayo atamlinda mtoto na kupata haki zake zote za msingi. Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Idara ya Ustawi wa Jamii, Siti Abasi Ali alipokutana na wadau kujadili umuhimu wa kufanya marekebisho ya sheria hiyo na kuja na sheria mpya itakayokidhi mahitaji ya msingi ikiwemo kumlinda mtoto.

Alisema sheria iliyopo ni ya takribani miaka 12, hivyo haiendani mabadiliko yanayoikabili Dunia ikiwemo sayansi na teknolojia katika mawasiliano.

Alisema sheria inayotumika kwa sasa imefanya kazi kubwa kumlinda mtoto na kupata haki zake za msingi, lakini mabadiliko yanahitajika kuona sheria inakidhi mahitaji ya msingi.

"Tunahitaji sheria ya kumlinda mtoto ambayo itakayoenda na wakati wa mahitaji yaliyopo kufuatia kuwepo kwa changamoto nyingi ikiwemo za sayansi na teknolojia katika masuala ya ushahidi," alisema.

Siti aliwataka wadau wa haki za watoto ikiwemo asasi za kiraia kushirikiana kwasababu huu ni wakati mwafaka wa kuona changamoto zote zinazojitokeza ikiwemo vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia zinashughulikiwa kikamilifu.

Alisema yamekuwepo majadiliano ya umri, matukio ya udhalilishaji wa kijinsia na ukuaji wa mtoto. "Mjadala huu ni mkubwa tunaziomba taasisi zote tunazofanya kazi katika mapambano dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia na ukuaji wa maendeleo ya mtoto tushirikiane kuona tunatoa maoni yatakayokuja na sheria mpya," alisema.

Hakimu wa Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Unguja, Khamis Rashid Khamis, alisema muongozo utawezesha utaratibu wa kusikiliza kesi zinazowahusu watoto katika umri upi ikiwemo miaka 11 hadi 16.

"Marekebisho ya sheria ya mtoto hayaepukiki zaidi katika kipindi hiki ambacho kuna mjadala wa umri wa mtoto kuanzia miaka mingapi zaidi katika matukio ya udhalilishaji wa kijinsia ikiwemo ubakaji," alisema.

Mchakato kuhusu umri wa mtoto umekuja baada ya kuwepo kwa majadiliano ya muda mrefu kwa wadau wanaojishughulisha na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia pamoja na wanawake na watoto zaidi katika adhabu.



WIZKID ANATIA HURUMA UKURASA 14

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT





# MPENI MAUA YAKE

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Ali Kiba amekuwa msanii wa kwanza kutoka Tanzania kutumbuiza katika mashindano makubwa ya soka yaliyoandaliwa na Shirikisho la mpira Duniani (FIFA) na lile la Afrika (CAF).

Kuteuliwa kwake kuwa mtumbuizaji katika ufunguzi wa michuano ya African Football League ni mwanzo mzuri kwake na sasa kuwa sawa na wasanii wakubwa waliotumbuiza katika mashindano makubwa duniani.

Wadau wa muziki nchini wanaeleza kwamba tukio hilo ni sawa na kupewa maua kutokana na kazi nzuri anayofanya, lakini iwe chachu kwake kwa kuendelea kupenya kimataifa.

Shukuru Karim, amesema kinachotakiwa kufanywa na msanii huyo ni kuhakikisha anatumia nafasi hiyo kupanda kisanii na sio kuanza kujisifu na kujigamba jambo ambalo halitamsaidia. “Kuteuliwa kwake kutumbuiza pekee ni alama ya kumheshimu na kumpandisha kisanii, sasa imebaki nafasi yake ya kuendeleza heshima aliyopewa,” amesema Karim.

Christopher Msekena, ameeleza tukio hilo litamfanya Ali Kiba kuonekana kila pande ya dunia, na atarajie kupata mialiko mingi ambayo akiitumia vyema atakuwa amepiga hatua zaidi.

“Kuna watu watamuona na kutaka kufanya nae kazi, kinachotakiwa atulie na kufanya maamuzi sahihi kwani akikosea hapo itakuwa tabu kwake,” amesema.

Ali Kiba miezi kadhaa nyuma alihamia Simba akitokea Yanga na imekuwa kama neema kwake kwani nafasi hiyo ya kutumbuiza kwenye ufunguzi angepata msanii mwingine mkubwa.

BASI SAWA

## ‘King of Diaspora’ yamtambulisha Ambri The Genius A.Mashariki


MSANII chipukizi wa muziki wa kizazi kipya anayeishi Marekani, Ambri The Genius, ametambulisha EP yake mpya na kujigamba kwamba ndio album fupi bora zaidi kwa wanamuziki wanaoishi nje ya nchi.

Ambri ambaye amekuwa akifanya muziki mchanganyiko wenye ladha ya Bongo Fleva, kwasasa anatamba na video ya wimbo Semezana kutoka kwenye EP hiyo yenye jina la King of Diaspora iliyotoka hivi karibuni.

Akizungumza na BT, Ambri amesema anafurahia EP hiyo yenye ngoma saba licha ya kuwa haina muda mrefu katika majukwaa kuuza na kununua muziki duniani.



## Lupita kawa singo tena



MSHINDI wa Tuzo ya Oscar, Lupita Nyong’o na mpenzi wake, Selema Masekela, wamevunja uhusiano wao baada ya kuwa pamoja kwa mwaka mmoja.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Lupita amesema bila kuweka wazi kwamba alihitaji kufichua ukweli huo wa kibinafsi na kujitenga na mtu ambaye hawezi kumwamini tena.

Lupita alizungumzia huzuni iliyokuwa ikimkabilia kutokana na penzi ambalo lilizimwa ghafla kutokana na udanganyifu.

Alikiri kwamba maumivu yake ya moyo yamempa mazingira magumu na maumivu.



## MARIOO UMESEMAJE VILE?

MKALI wa amapiano nchini, Marioo amesema hakukosea kumshirikisha mkongwe Mr Nice katika wimbo wake mpya ‘Shisha’ ambao kwa sasa umewashika mashabiki.

Amesema tangu zamani alikuwa akimpenda mwanamuziki huyo, hivyo kibao hicho anataka kuwakumbusha vijana kuwa miaka ya nyuma alikuwa msanii Mr Nice ambaye hadi leo kipaji chake bado kipo juu.

“Mr Nice kwangu sawa na nembo niliyoipenda na ndio maana nikaamua kufanya naye kazi ya pamoja, nataka matunda haya aliyohangaika kuyamwagilia aendelee kunufaika nayo,” amesema Marioo.



## Meja Kunta mguu mmoja nje

KIBAO kipya cha mwanamuziki wa Singeli, Meja Kunta kinachoitwa Chuu, kimeonyesha jinsi muziki huo ukifanyiwa mageuzi unaweza kuvuka mipaka na kupendwa na mashabiki wengi wa muziki.

Ndani ya wimbo huo Meja Kunta ameshirikiana na wanamuziki wakali Baba Levo na Ntoshi Gazi kutoka Afrika Kusini.

Ntoshi Gazi amefanya kazi na wanamuziki wakubwa wa Bongo Fleva hapa nchini akiwamo Diamond Platnumz, Rayvanny na Whozu.

## TUMEWAMISS KWENYE HIP HOP

**Na Adam Fungamwango**

NI kama muziki wa kufokafoka maarufu kama ‘hip hop’ umeanza kufifia kwenye gemu la muziki bongo, ingawa kuna wasanii kadhaa wanakomaa ili kuendelea kuwepo.

Muziki wa bongo fleva kwa sasa ambao staili yake ni kuimba zaidi kuliko ‘kuchana’ ndiyo ulioonekana kumeza muziki huo.

Wasanii kama Roma Mkatoliki, Stamina, Nay wa Mitego, na Dogo Janja, ndiyo angalau wanaufanya uendelee kuishi.

Leo tunawakumbuka wasanii wa muziki huo waliotamba kuanzia miaka ya 2000 na kuufanya muziki huo kufanya vema kwenye soko la muziki Tanzania.

**Mwana FA**

Kwa sasa ni Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Hamis Mwinjuma, maarufu kimuziki kama Mwana FA, ni mmoja wa wasanii waliokuza muziki wa bongo fleva, hasa wenye mahadhi ya hip hop.

Ndiye msanii aliyekuwa akileta misemo mingi iliyokuwa ikitumika uswahilini, maarufu kama ‘uswazi’ kutokana na ngoma zake nyingi kujikita kwenye visa na mikasa ya kijamii zaidi kama vile ‘Bado Nipo Nipo’, ‘Uninijua Unanisikia?’, ‘Unanitega’, ‘Habari Ndiyo Hiyo’, na nyingine nyingi.

Pia ni Mbunge wa Jimbo la Muheza, hivyo kwa sasa anatumikia zaidi wananchi, huku mashabiki wa muziki wake wakiwa wamemmisi sana na ngoma zake za zilizokuwa zikizalisha misamiati uswazi.

**Joseph Mbilinyi ‘Mr 2 Sugu’**

Ni mmoja kati ya waasisi wa muziki huo wa kufokafoka, tangu wakati baadhi ya watu hawauelewi vizuri na kuonekana kama wa watu wakorofi, wahuni.

Yeye na Joseph Haule maarufu kama ‘Profesa Jay’, na wengine wachache, walikomaa na kubadilisha aina ya maudhui ya nyimbo na kuimba vitu ambavyo vilianza kuwakuna hata watu wazima na kuanza kuukubali muziki huo, ulikuwa ukiangazia zaidi matatizo ya kijamii zaidi, badala ya mapenzi.

Lakini kasi ilipungua baada ya kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini miaka kadhaa nyuma, na hata alipoondoka kwenye ubunge amebaki zaidi kwenye nafasi ya uanasiasa kuliko muziki, hapo mara moja moja anakumbushia.

Nyimbo kama ‘Wananita Sugu’ na ‘Sugu Moto Chini’ zilimtangaza na kumfanya ajizolee mashabiki wengi.

**Profesa Jay**

Kwa hakika huyu ndiye aliyebadilisha aina ya ‘meseji’ kwenye muziki wa ‘hip hop’ ambapo awali zilionekana kama ni za kihuni, lakini alizungumzia maisha ya kila siku kwenye jamii, kwa kiwango kilichowafanya hata watu wazima kuanza kuukubali muziki huo.

Ngoma kama ‘Ndiyo Mzee’, ‘Bongo Dar es Salaam’, ‘Zali la Mentali’ zilimfanya kuwa maarufu.

Akaja kuwa Mbunge wa Jimbo la Mikumi. Kwa sasa si mbunge tena. Alionekana kuanza kurejea kwenye gemu, lakini akakwamishwa na maradhi ambapo kwa sasa amepona na anapambana kurejea kwenye hali yake ya kawaida.

**Inspekta Haroun**

Aliufanya muziki wa hip hop kupendwa hata na kinadada kutokana na aina yake ya utunzi.

Marapa wengi kupenda zaidi kuimba nyimbo ngumu, za kijamii, kisiasa na uchumi, lakini Inspekta Haroun alifanya mabadiliko kidogo na kutunga nyimbo za mapenzi kwa mtindo huo wa hip hop.

Nyimbo kama ‘Asali wa Moyo’ na ‘Mtoto wa Geti Kali’ ziliondokea kupendwa na kumfanya kuwa mmoja wa wasanii maarufu sana mwanzoni mwa miaka ya 2000.

**Afande Sele**

Alitawazwa kuwa mfalme wa Rhymes, aliposhinda kwenye shindano hilo mwaka 2004 jijini Dar es Salaam, akiwashinda wasanii wengi maarufu wa muziki huo waliokuwepo wakati huo.

Ni rapa mkongwe nchini ni mmoja wa wasanii waliochangia kuufikisha muziki wa hip hop hapa ulipo.

FILAMU

## Binti Mfalme: Ikiandikwa haifutwi

**Na Adam Fungamwango**

BINTI mfalme ni filamu inayomhusu kijana mmoja aitwaye Evance ambaye alitoka mjini kwenda kijijini kumtembelea bibi yake, lakini anakutana na mkasa ambao atauelezea katika maisha yake yote.

Filamu imechezwa na Dunia Mkate kama Evance, Diana Emmanuel akicheza kama binti mfalme, Shaaban Issa akiwa Mfalme Kagongo, Zainabu Maduka akicheza kama Bi Luku, Omari Mustapha, akiwa kama mfalme Nyori.

Evance anafika kijijini kwa bibi yake, lakini ni moja kati ya vijiji vya himaya inayotawaliwa na mfalme Kagongo.

Mfalme huyo ana dada yake ambaye ni binti mfalme. Binti huyo baada ya kumuona Evance tu, anatokea kumpenda.

Kabla ya hapo alikuwa ameshachumbiwa na mfalme Nyori na anarajiwa kuolewa. Mila za himaya zote za huko ni kwamba watu wa familia za kifalme huolewa au huoa kwenye familia za lofalme pia.

Binti akamwambia kaka yake kuwa hataki kuolewa na mtu yoyote isipokuwa Evance. Mfalme Kagongo alikasirika sana. Lakini pia kijana huyo alikuwa anakabiliwa na kosa lingine la kukiuka mila na desturi za kijiji hicho kutokana na aina ya nguo alizokuwa amevaa. Ni za kimjini zaidi.

Anawatuma walinzi wake kwa siri wakamuue kijana huyo. Kwa bahati nzuri binti anasikia amri hiyo na haraka akakimbia mpaka kwa Bi. Luku ambaye ni bibi yake Evance. Badala ya kumwambia akimbie, anamshika mkono na kumwambia wakimbie wote.

Wanakimbia porini kwenye msitu mkubwa ambako wanakaa huko kwa siku kadhaa kabla ya kukamatwa. Walinzi wa mfalme Nyori ndiyo wanaowakamata. wanapelekwa kwenye mpaka wa himaya zote mbili. Mfalme Kagongo anaitwa kwenda kumuona dada yake na hawara yake.

Wanasomewa mashtaka yao, lakini Evence ndiye anayehukumiwa kifo na binti mfalme kuachia kwa sababu damu nzito kuliko maji.

Gafla anaingia mgeni ambaye hawamtambui. Anajitambulisha kama ni kaka wa Evance ametoka mjini baada ya kuambiwa mdogo wake yupo kwenye matatizo.

Anawaomba radhi wafalme wote wawili na kuahidi kulipa gharama na fidia zote watakazozitaka kwa sababu ana uwezo. Wafalme tamaa inawaingia na kila mmoja kutaja fidia yake na gharama anazozitaka.

Evance anaachia huru, anapewa mchumba, kaka anaamua kuwachua wote wawili na bibi yao kuwapeleka mjini kwa sababu kwenye himaya hizo kumeshachafuka.





# Jada, Smith wahaha kurudisha penzi

MWIGIZAJI wa Marekani, Jada Pinkett amesema yeye na mume wake Willy Smith walijaribu kurudisha uhusiano wao, lakini ilishindikana.

Pinkett Smith katika mahojiano ya hivi karibuni katika kipindi cha The Morning Show amesema ingawa yeye na Smith wametengana kwa miaka saba iliyopita, lakini wanafanya kazi na kujaribu kuifufua. Alipoulizwa ikiwa wangeachana, alisisitiza kwamba hakukuwa na talaka ya karatasi au kwa nadharia.



## Halle Baille mama kijacho?

MWIGIZAJI kutoka Hollywood, Halle Bailey ameonekana hadharani akiwa na tumbo kubwa na kuibua fununu kwamba ni mjamzito.

Katika mfululizo wa picha zilizopigwa kuanzia Oktoba 16, zinamuonyesha mwigizaji huyo akitembea na mpenzi wake wa rapa, DDG akiwa amevalia nguo pana.


Ingawa alivalia mavazi mapana ya rangi ya kijivu, kile kilichoonekana kama ujauzito kilionekana kwa urahisi alipokuwa akitembea kwenye mitaa ya Santa Monica.


## Davido alipata mshtuko

STAA wa muziki wa Nigeria, David Adeleke, maarufu kama Davido, amefichua kwamba yeye na mkewe, Chioma Rowland, walipatwa na hali ya kutetemeka walipogundua kuwa walikuwa na watoto mapacha.

Nyota huyo amesema hayo wakati wa mahojiano ya hivi majuzi kwamba imani yake ilitetereka baada ya kufiwa na mtoto wake wa kiume mwenye umri wa miaka mitatu, Ifeanyi.

"Mimi na mke wangu tulipogundua, tulikuwa tunatetemeka na ilikuwa mwezi huo huo, ilitokea Oktoba na mke wangu alijifungua Oktoba, ni kama wazimu." Amesema Davido.





## Wizkid anatia huruma

MWANAMUZIKI wa Kimataifa, Ayodeji Balogun, anayejulikana kama Wizkid, ameweka picha akionekana akishiriki ibada ya mazishi ya mama yake mzazi.

Mama yake Jane Dolapo, alizikwa katika hafla ya kifamilia Oktoba 13, mwaka huu.

Katika video nyingi zilizosambaa kwenye mitandao ya kijamii kutoka katika ibada hiyo alionekana Wizkid akiwa amezidiwa na huzuni.

## Utata sumu iliyomuua Mohbad

MWIGIZAJI wa Nollywood, Iyabo Ojo, amefichua kuwa Jeshi la Polisi la Nigeria bado linasubiri matokeo ya sumu iliyogundulika kutoka katika uchunguzi wa maiti ya mwimbaji wa Nigeria, Mohbad, ambaye aliyefariki Septemba 12, mwaka huu.

Mwigizaji huyo aliandika kwenye Instagram Oktoba 17, amefichua kuwa mwili wa mwimbaji huyo bado haujatolewa hospitalini tangu ulipofukuliwa mnamo Septemba.

Ojo pia alibainisha kuwa kamera za CCTV katika nyumba ya Mohbad zilizimwa na hivyo hakuna picha zilizoonyesha matukio mbalimbali ikiwamo kabla ya ya kifo chake.





# Madiwani watoa ya moyo ujenzi miradi ya maji

**Na Dege Masoli,** KILINDI

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga, wameonyesha wasiwasi wao kusuasua kwa utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo yao kwa wakati na kupoteza maana ya kumtua mwanamke kichwani ndoo ya maji.

Diwani wa Kata ya Mvungwe, Abdalah Ndaro, aliibua hoja ya mradi wa maji uliogharimu zaidi ya Shilingi milioni tano akidai haujaleta manufaa kwa wapigakura wake.

Ndaro, aliibua hoja hiyo katika mkutano mkuu wa wadau wa sekta ya maji wilayani Kilindi ulioandaliwa na Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA).

Diwani Ndaro, alisema licha ya mradi huo kukamilika, haujaleta tija kwa wananchi kwa sababu maji yake ni machungu, hivyo hayafai kwa matumizi ya binadamu.

Diwani wa Kata ya Kibirashi, Bakari Fau, alieleza kukerwa na miradi ya maji kuchukua muda mrefu kukamilika na kudai unaondoa maana ya kusudio la kumtua mwanamke ndoo kichwani.

"Maneno usanifu na manunuzi kwenye miradi ya maji hapa wilayani kwetu yamekuwa kikwazo cha miradi kutekelezwa kwa wakati, sielewi ni kwetu tu au hata kwa wenzetu wa wilaya nyingine? "Alihoji

Diwani wa Kata ya Kilindi Asilia, Juma Bewa, aliishauri Ruwasa kuunda vyombo vya kusimamia huduma ya maji kwa wakati ili kuweza kuingia kwenye mpango wa lipa kwa matokeo ambao fedha zake zimeelekeza kuwa ni miongoni mwa sifa za kuzipata.

Awali katika taarifa ya RUWASA iliyosomnwa na Kaimu Meneja Wilaya ya Kilindi, Abdalah Issula, Shilingi bilioni 3.3 zitatumika kwenye miradi ya maendeleo ya maji kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Kwa mujibu wa Issula, miongoni mwa changamoto wanazokabiliana nazo ni pamoja na ukosefu wa vyanzo vya maji vya uhakika na uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli za kibinadamu za ukataji miti ovyo na kilimo kwenye vyanzo vya maji. Aliitaja miradi mitano inayotekelezwa kwa msimu huo kuwa ni wa maji Mafisa, Bokwa, Mafulila, Mabaranga na uchimbaji visima 23 Kata ya Kilindi Asilia. Miradi mingine mitatu ni Songe,Diburuma, Saunyi na Msente.

Akitoa mada iliyohusu uimarishwaji wa vyombo vya maji (CBWSO) katika usimamizi, uendeshaji na utoaji wa huduma ya maji ngazi ya jamii, Hance Israel kutoka Ofisi ya RUWASA Mkoa wa Tanga, alieleza umuhimu wa vyombo hivyo kusajiiwa, kuvijengea uwezo wa kujiendesha na kutekeleza sera ya maji na sheria zake.

Hata hivyo Israel alielezea wajibu wa jamii kulipia huduma ya maji kwenye maeneo yao ili kuifanya kuwa endelevu na hivyo kuwezesha kufikiwa kwa lengo la asilimia 100 kupata maji ifikapo mwaka 2030.

Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Kilindi, Michael John,ambaye ni Ofisa Tarafa, aliwataka viongozi kuanzia ngazi ya kijiji na kata kudhibiti uharibifu wa mazingira ikiwemo kuwachukulia hatua wanaojihusisha na vitendo hivyo, vinginevyo watawajibika.

# Daktari bingwa, mtaalamu wa usingizi wasimamishwa kazi

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu amemsimamisha kazi daktari bingwa, mtaalamu wa usingizi na muuguzi wa chumba cha upasuaji kwa tuhuma za kukwamisha utoaji huduma kwa wananchi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga ya Bombo.

Uamuzi huo ulitangazwa juzi jijini hapa na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Godwin Mollel baada ya kufuatilia malalamiko ya wananchi kukosa huduma bora za afya katika hospitali hiyo.

"Tunaendelea kufanya uchunguzi katika idara zote za Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga Bombo na watumishi wengine 26 nao wanaendelea kuchunguzwa zaidi," alisema Dk. Mollel.

Ametoa onyo kali kwa madaktari wa hospitali za serikali nchini kuacha tabia za kutoa rufaa kwa wagonjwa kwenye hospitali zao bila sababu za msingi za matibabu na kuwapelekea hospitali binafsi.

Kwa upande wa wamiliki wa hospitali binafsi nchini, alisema wanatakiwa kufuata taratibu na kanuni zilizopo kuendesha hospitali zao na kuonya atakayebainika kuwarubuni madaktari wa hospitali za serikali kutoa rufaa bila sababu ya msingi atachukuliwa hatua za kisheria.

"Sio kwamba tunawakataza madaktari wa Serikali kufanya kazi baada ya muda kuisha lakini isiwe muda wao wa kazi wanakwenda kufanya kazi hospitali binafsi na kusababisha wagonjwa kukosa matibabu katika hospitali za serikali," alisisitiza

Vilevile, aliwakumbusha watumishi wa afya nchini kipaumbele cha Rais Samia Suluhu Hassan kuwa ni huduma bora za afya kwa wananchi wote bila kujali hali zao za uchumi.



Mgombea nafasi ya Mwenyekiti wa Chama cha Kulinda na Kutetea Haki za Walimu Tanzania (CHAKUHAWATA), wilaya ya Muheza, Theraphin Mvungi akizungumza wakati akiwashukuru wajumbe kwa kumpitisha bila kupingwa katika uchaguzi mkuu, mjini Muheza mkoani Tanga jana. Wengine waliopita bila kupingwa ni Katibu wa wilaya, Tumaini Peter, Mwakilishi wa walemavu, Mariam Hamadi na Mwakilishi wa Taasisi ya elimu, Festo Mnkeni. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Viwanja vya ndege vyabanwa gawio kwa serikali

**Na Mary Mosha,** HAI

VIWANJA vya ndege nchini, vimeagizwa kujitathimini katika uendeshaji na kutoa gawio la faida ya fedha kwa Serikali.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, David Kihenzile wakati wa ziara yake ya kikazi katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) uliopo wilayani Hai.

Vilevile aliigiza Kampuni ya Uendeshaji Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro (KADCO) kuongeza ukusanyaji mapato kwa kuongeza idadi ya mashirika ya ndege zinazotua katika uwanja huo. "Viwanja vyote vya ndege nchini, hakikisheni mnalipa mishahara wafanyakazi, mnajiendesha bila hasara, kutoa huduma bora na gawio kwa Serikali," alisema Kihenzile na kusisitiza kuwa:

"Acheni ulemavu wa kuisubiri Serikali iwasaidie. Kuna miradi mingi ya elimu, afya, maji na barabara inahitaji fedha kwa ajili ya usimamizi, hivyo kila mmoja atekeleze wajibu wake na kuwa wabunifu. Alisema pamoja na KIA kuwa na mikakati mingi, hataki kuona tatizo la kuendelea kuwepo kwa tatizo la kuzimika taa mara kwa mara linaendelea kutokea uwanjani hapo. "Sitaki kuona matatizo kama yale ya kuzimika taa uwanjani hali inayopelekea baadhi ya ndege kupata matatizo... lazima mtekeleze maagizo yote ya viongozi wa ngazi za juu kwani kila mmoja anania njema na kiwanja hiki."alisema.

Aliwataka makandarasi waliokabidhiwa miradi katika viwanja vya ndege nchini kuhakikisha wanakamilisha kwa wakati na kwa viwango vya ubora uliokusudiwa.

"Nimetembelea chumba cha kuhifadhia vyakula kabla ya kupelekwa nje ya nchi, maboresho makubwa yanaendelea, kazi imebaki kwa wakulima kuhakikisha wanalima kwa ubora na tija zaidi, wafugaji wawe na mtazamo chanya kwa kuuza nje ya nchi, hii itasaidia kukukuza uchumi wa watu wetu, Ongezeni ndege za mizigo, angalieni wengine wanafanya nini, lengo ni kuongeza tija na ajira," alisema.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Kumbuka zama mastaa picha za Kihindi, Amitabh Bachchan, Mithun Chakraborty

## -Ubabe wao, 'masongi', mbwembwe za uchezaji...

**Na Adam Fungamwango**

ILIKUWA ni mshikemshike siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili wakati vijana, watu wazima wake kwa waume walipokuwa wakitoka majumbani kwao kwenda majumba ya sinema kuangalia filamu mbalimbali.

Hiyo ni miaka ya 1970 hadi mwishoni mwa 1980. Wakati huo Tanzania haikuwa na televisheni wala video.


Kwa Dar es Salaam, majumba yaliyokuwa maarufu ilikuwa ni Drive Inn Cinema. Jumba hili lilikuwa maarufu kwa sababu hata vijana, watoto wa uswahilini kama Mwananyamala, Kinondoni, Manzese, Mburahati, Ubingo, Mabibo, Tandale, Magomeni waliweza kuangalia filamu bila malipo yoyote.

Bodi lake ya kuonyesha picha lilikuwa juu mno ambapo lilionekana na mtu yeyote wa maeneo ya Msasani.

Sehemu hiyo ni pale ambapo hivi sasa umejengwa Ubalozi wa Marekani, na hadi leo makonda wa daladala wa maeneo hayo wanaitia abiria 'Drai Chama.'

Ndiyo ilikuwa sehemu pekee watoto wa uswazi waliangalia picha bure, ambapo ujenzi wake ulitofautiana na majumba mengine ya sinema, kwani bodi lilikuwa juu, halafu umezungushwa ukuta kama Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, ambapo wenye pesa wanakata tiketi kuingia ndani, humo utakutana na sauti na huduma nyingine kama siti, vyakula, vitafutwa, lakini wanaokuwa nje ya ukuta wanaona, ila bila kusikia sauti. Na hili wala halikuwasumbua. Waliangalia picha ambazo zilikuwa zinaanzia saa 12:00 jioni hadi saa 3:00 usiku, haooo nyumbani.

Majumba mengine, ambayo hayo sasa hayakuwa ya dezo,




unakata tiketi na kuingia ndani, ni Cameo, Empress, Empire, Avalon, New Chox, Starlight na zingine.

Mikoani nako kulinoga, kwa sababu kulikuwa na majumba maeneo mbalimbali, kila mkoa ulikuwa na jumba maarufu la sinema.

Miaka ya 1990 wakati TV na video zake zilipoanza kuingia na majumba ya starehe kuanza kufa kifo cha kawaida, kuna maeneo ya majumba ya watu binafsi yalianza kufanya kazi hiyo.

Kwa Dar hasa Wilaya ya Kinondoni, hasa watoto walikuwa wakienda kuangalia sinema sehemu moja inaitwa Milano, Magomeni Makanya, na Magomeni Morocco, nyumba moja mkabala na Kanisa Katoliki Mashahidi wa Uganda.


Purukushani zote hizo, pamoja na picha zingine watu walikuwa wagonjwa mno na picha za Kihindi, wenyewe waliziita za Kidosi.

Kulikuwa na mashindano na mabishano kila mmoja akimpenda 'stelingi' wake. Hawa ndiyo mastaa waliotamba sana kipindi hicho.

**AMITABH BACHCHAN**

Unaweza kusema huyu ndiye staa namba moja aliyekuwa akipendwa wa mashabiki wengi wa muvi za Kihindi nchini. Alizaliwa Oktoba 11, 1942, akiwa na miaka 81 sasa.

Pamoja na kwamba alianza 'kuekti' picha miaka ya 1969 na kuendelea, lakini alikuja kuwa staa na kipenzi cha watu duniani wa picha za Kihindi kuanzia mwaka 1975 na alitamba hadi 1988, walipoanza kuja mastaa wengine, ingawa alibaki na heshima yake.




Kwa hapa Bongo picha ambayo imeweka kwenye kumbukumbu ni Andha Kanoon au kwa Kiswahili 'Sheria Kipofu', ambayo ilikuwa ikiwafanya watu kuangua kilio kutokana na maudhui yaliyomo, iliyoachiliwa mwaka 1983.

Movi zingine ni Bombay to Goa, Shakti, Dostana, Naseeb, Mahaan, Jaadugar, Shahenshah Namak Halaal,Aakhree Raasta, Inquilaab, Sharaabi, Aakhree Raasta na nyingine nyingi.

**MITHUN CHAKRABORTY**

Kwa kiasi kikubwa staa huyu ndiye aliyekuja kuwa mpinzani mkubwa wa Amitabh. Alianza kukubalika wa Wabongo kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 1980 na hasa muvi yake iliyokonga nyoyo ni Disco Dancer iliyotetemesha kila jumba la starehe. Movi hii ilifyatuliwa mwaka 1982.

Jamaa huyo aliyezaliwa 16 Juni 1950, akiwa na miaka 73 sasa alicheza filamu nyingi kali ambazo ni Jaal, Commando, Charnon Ki Saugandh, Baazi, Dance Dance, Mera Yaar Mera Dushman, Deewana Tere Naam Ka, Cheetah, Bhishma, Loha, Kaalia na nyingine kadhaa.

**GOVINDA**

Jina lake kamili ni Govind Arun Ahuja, aliyezaliwa mwaka 1963 na kwa sasa ana miaka 59.

Huyu alianza kutamba miaka ya mwanzoni mwa 1990, akicheza picha kama vile Raja Babu, Taaqatwar, Sachai Ki Taqat, na Dost Garibon Ka.

Wabongo wanamfahamu mwamba huyu kwa kazi yake aliyoifanya kwenye filamu ya 'Hatya,' iliyotolewa mwaka 1988.

Wengi wanaifahamu kwa jina la 'Yaya' ambalo ni ni neno la pekee la analoweza kuongea mtoto mwenye changamoto ya kuongea 'bubu' kwenye picha hilo.

**SUNNY DEOL**

Mmoja wa wababe wa picha za Kihindi aliyejichukua umaarufu mkubwa kwa vijana wa miaka ya 1990 hadi mwanzoni mwa 2000.

Jamaa amerithi kazi ya baba yake. Ni mtoto wa mbabe mmoja wa filamu za kihindi miaka ya nyuma aitwaye Dharmendra.

Alitamba na filamu kama, Arjun, ChaalBaaz, Ajay, Ziddi, Indian, Kasam na nyinginezo.

Alizaliwa October 19, 1957 akiwa na miaka 66 sasa.

**AKSHAY KUMAR**

Ni mmoja wa mastaa aliyekuwa na mashabiki wake wengi hapa Bongo kutokana na kazi yake nzuri ya uigizaji wa picha za kibabe kuanzia miaka ya 1990.


Alizakuwa Septemba 9, 1967, ana miaka 56 sasa akiwa amecheza picha kadhaa zilizopendwa na wengi kama, Dil Ki Baazi, Mohra, Paandav, Jaanwar, Dil To Pagal Hai na nyingine nyingi.

**SUNIEL SHETTY**

Mbabe huyu wa mangumi alizaliwa Agosti 11 mwaka 1961. Ana miaka 62 sasa. Jamaa wanamkubali sana Bongo kutokana na muvi zake za kibabe na kutochelewesha mambo. Huwa haulizi mara mbili mbili.

Filamu zake ni Dilwale, Mohra aliyecheza na rafiki yake kipenzi Akshay Kumar kwani baadhi ya picha kadhaa wamecheza pamoja, Krishna, Vinashak na zinginezo.

**Tuma meseji 0716 350534**



# Vifo vyafikia watu 3,785 Gaza, Israel yaendelea kuichimbua

**GAZA, Palestina**

ISRAEL imeendelea kushambulia ukanda wa Gaza usiku kucha wa jana na kusababisha ongezeko la watu waliouawa kufikia 3,785.

Jeshi la Israel lilisema ndege zake za kivita zilishambulia maeneo zaidi ya 100 na kumuua mwanachama mmoja wa Hamas ambaye inaaminika huenda alishiriki katika uvamizi uliofanyika Oktoba 7 uliosababisha vifo vya watu 1,400 nchini Israel.

Kwa upande mwingine, mamia ya watu waliandamana mjini New York, Marekani wakiomba kuachiwa huru mateka wa Israel waliochukuliwa na Hamas.

Akihutubia umati huo, Balozi wa Israel katika Umoja wa Mataifa, Gilad Erdan, alimkosoa Katibu Mkuu wa Umoja huo, Antonio Guterres, kwa kuweka msisitizo kwenye misaada ya kibinadamu kwa watu wa Gaza badala ya kuachiwa huru kwa mateka.

"Marafiki, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa atatembelea kivuko cha Rafah huko Gaza. Hivi sasa, cha kusikitisha, inaonekana kwamba kipaumbele chake kikuu ni kutoa misaada kwa magaidi, magaidi waliowateka nyara wapendwa wetu. Aibu kwake." Alisema Erdan.

Akiwa mjini Cairo nchini Misri kutazama maandalizi ya msaada utakaopelekwa kwa Wapalestina kwenye Ukanda wa Gaza, Guterres alisema eneo hilo linahitaji msaada wa kutosha na wa kudumu huku akitoa pia wito wa usitishaji mapigano mara moja kwa ajili ya misaada ya kiutu

Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa, Philippe Lazzarini alisema mashariki ya kati iko kwenye hatari ya kutumbukia shimoni kutokana na vita kati ya Israel na Hamas.

Kamishna huyo mkuu wa shirika la misaada la Umoja wa Mataifa (UNRWA) alisema ghasia zinaweza kusambaa katika eneo lote.

Alionya juu ya hali mbaya kwa raia ndani ya Gaza, akitoa wito tena wa kutolewa kwa misaada ya kibinadamu katika eneo hilo.

Lazzarini alisema anahofia dunia inapoteza utu wake.

Katika mahojiano ya kipekee na BBC, Lazzarini alikariri wito wa maeneo ya kutoa misaada ya kibinadamu, akisema msaada unahitaji kutoingiliwa ili kusaidia watu wa Gaza.

Akizungumza mjini Jerusalem, Lazzarini alilaani mashambulizi yaliyofanywa na Hamas dhidi ya Israel, na kuyataja kuwa ni mauaji ya kutisha na ya kinyama ambayo yamezua taharuki kitaifa. "Lakini tukio hili bado halihalalishi kwamba vita vinaendeshwa bila kizuizi chochote," alisema.

Alipoulizwa iwapo Waisraeli wanaheshimu sheria za kimataifa za kibinadamu, Lazzarini alisema: "Sikiliza, sasa tuko katika hali ambapo Ukanda wa Gaza umezingirwa kabisa.

Tuko katika hali ambayo zaidi ya watu milioni moja wametakiwa kuhama makazi yao. Hivyo hii ni sawa na adhabu ya pamoja, na adhabu ya pamoja ni ukiukaji wa sheria za kimataifa za kibinadamu."

**BBC**

## Kiongozi aliyepinduliwa alitaka kutoroka kuzuizi

**NIAMEY,** NIGER

SERIKALI ya kijeshi nchini Niger imesema imezuia jaribio la kiongozi aliyeondolewa madarakani, Mohamed Bazoum, kutoroka kizuizini.

Msemaji wa serikali alisema rais huyo wa zamani alijaribu kutoroka usiku na familia yake, wapishi na wana usalama wake.

Kulikuwa na mipango ya kundi hilo kwenda nchi nyingine kwa kutumia helikopta lakini mpango huo uligundulika, aliongeza.

Bazoum amekuwa chini ya kizuizi cha nyumbani tangu wanajeshi wa kikosi cha rais kufanya mapinduzi mwishoni mwa Julai.

Niger ni sehemu muhimu ya kanda ya Afrika inayojulikana kama Sahel, ukanda wa ardhi unaoanzia Bahari ya Atlantiki hadi Bahari ya Shamu.

Eneo hilo linasumbuliwa na wanamgambo wa jihadi na limezingirwa na tawala za kijeshi.



Hali ilivyo kwenye kambi ya wakimbizi ya Jabalia, Ukanda wa Gaza, katika picha iliyochukuliwa Oktoba 11 mwaka huu. **PICHA: GETTY IMAGES**

# Wanne wafariki dunia kwenye mkanyagano

**NAIROBI,** KENYA

WATU wanne wamefariki dunia katika mkanyagano wa msongamano uliotokea wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mashujaa nchini Kenya.

Tukio hilo limetokea majira ya asubuhi ya jana wakati watu waliosongamana wakitaka kuingia ndani ya uwanja kushuhudia maadhimisho hayo.

Polisi nchini humo imethibitisha kutokea kwa vifo hivyo vilivyosababishwa na mkanyagano huo.

Rais William Ruto aliongoza taifa hilo kusherehekea Siku ya Mashujaa na kutilia mkazo uwepo wa mpango wa afya bora kwa wote. Kiongozi huyo alizinduwa mpango mpya wa huduma ya afya kwa wote uitwao "Afya Nyumbani" wakati wa maadhimisho hayo yaliyofanyika mjini Kericho.

Uzinduzi huo unafuatia hatua ya rais huyo kuidhinisha sheria nne mpya, ambazo zingetumika kuendesha shughuli za afya nchini kote.

Rais Ruto alisema serikali yake imetenga shilingi bilioni tatu kila mwaka kwa ajili ya mpango huu.

Serikali ya Kenya ilisema inatilia mkazo kuzuia magonjwa na vile vile kuwapa nafasi wananchi wote kuchangia mfumo mpya wa afya.

"Wahamasishaji wa afya 100,000 watakaotekeleza mfumo huu mpya wameshapewa vifaa vya matibabu, na watapewa simu za kisasa kuwawezesha kufuatilia wagonjwa, kuweka rekodi na kuwasiliana na wizara husika kwa haraka panapokuwa na uhaba wa madawa au matatizo yoyote." Alisema Rais Ruto.

Hata hivyo, viongozi waliohudhuria kwenye sherehe hiyo walijikuta wakiingiza sioasa katika hutuba zao kwa kuzingatia sherehe hiyo ilifanyika katika ngome ya Rais Ruto.

Naibu Rais Rigathi Gachagua alichukau fursa hiyo kuonyesha nguvu za serikali yao, akiwakosoa wapinzani kwa kutokuwa na mawazo ya kimaendeleo.

Sherehe hiyo ilivutia umati mkubwa wa watu, baadhi yao wallala nje ya uwanja ili kuwapa nafasi ya kuwahi kuingia ndani.

**DW**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

ISSA HASANI SONGA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 461 AYY – TOYOTA HAICE CS/CUSTOM. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: KW/RB/4860/2023.

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 138 OF 2023
In the matter of the Estate of the late VENETHIA OBED MTUI of Kilimani within Dodoma City
AND
IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY
ALPHA PETER SHAYO AND HELEN PETER SHAYO

**GENERAL CITATION**
(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 25 Day of 10,2023
Dated at Dodoma this 17 Day of 10, 2023

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

NANCY JAMES LYAKURWA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 624 DCD – TOYOTA VITZ yenye Chassis No. KSP905015402. Engine No. IKR123943. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: PHQ/ARU/ARU/4771/2023

## KUPOTELEWA NA CHETI



SARAH MLANGI anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1163/0019 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MAMA SITTI MWINYI SEKONDARI mwaka 2002. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: PHQ/DAR/KIN/28679/2023.

## KUPOTELEWA NA CHETI



JIMMY PETER MSIGWA anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0531/0067 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia RUAHA SEKONDARI mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: PHQ/IRI/IRI/2288/2023.

3FORM 58
IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE
AT ONE STOP CENTRE
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1108 OF 2023
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GWAKISA GILBERT MWAISUMO
AND
IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION
BY ANNA WILSON MWAKIBETE
GENERAL CITATION
(Rule 75)

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 7th day of NOVEMBER, 2023.
Dated at DAR ES SALAAM this 17th Day of OCTOBER, 2023

*Senior Resident Magistrate*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
ILIYOPO MOROGORO
TANGAZO LA KUITWA SHAURINI
SHAURI LA MADAI /TARAKA/MIRATHI NAMBA 42/2023
MDAI/MUOMBAJI/MSIMAMIZI: FLORINA FRANCIS
DHIDI YA
MDAIWA: JEREMIA RICHRD MSHANDETE

KWA;JEREMIA RICHARD MSHANDETE WA MOROGORO

OMBI LA MDAI : FLORINA FRANCIS wa KOLA (A)
MADAI YA TALAKA 42/2023

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri lilimepangawa kusikilizwa mnamo tarehe 24 Mwezi 10 Mwaka 2023 saa 2:30 Asubuhi .
Angalia kama hukudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii inaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 17/10/2023

FOMU MIRATHI - 2
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TANGA
Kituo cha MJINI TANGA Mkoa wa TANGA
Usimamizi wa Mirathi Na. 173/2023
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU NG'ANZI MWALIMU NG'ANZI
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA
NA SELEMANI NG'ANZI MWALIMU
TANGAZO
(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 26 mwezi 10 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetokewa leo tarehe 03 mwezi 10 mwaka 2023.

HAKIMU

## KUPOTELEWA NA CHETI



FELICIAN KAIZILEGE WILBARD, Anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha NNE chenye index no S0624-0076 kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia shule ya sekondari RUBALE Mwaka 2020, Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
TAARIFA YA POLISI: PHQ/KAG/BUK/1117/2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 197/...2023**
**MDAI: MAGESA JULIUS KAMBARAGE**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: NICHOLAUS MARTINE**

KWA: NICHOLAUSI MARTINE
KIHONDA -MKUNDI
Ombi la mdai :MAGESA JULIUS KAMBARAGE,MADAI YA TSHS.1,290,000/=
Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri lilimepangawa kusikilizwa mnamo tarehe 23 Mwezi 10 Mwaka 2023 saa 8:30 Asubuhi .
Angalia kama hukudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii inaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 18/10/2023

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

ELIAS BENJAMINI MKWIZU Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 965 EDY FOLESTER SUBARU. Chasses Namba SH5-024437, Engine Namba EJ20D630813 Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
Polisi Taarifa : PHQ/ KIL/HAI/3145/2023

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701*

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumbani moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

## MAITI KWENYE KIROBA-31

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Charton alitua Uwanja wa Ndege Julius Nyerere Dar es Salaam na kwenda moja kwa moja Banana akaungana na Patauli, kumtesa mkewe, kumuonyesha picha za yule mpenzi wake wa zamani Burton, kumuuliza maswali ya kipuuzi, wakamfanyia ukatili mkubwa, wakaanza kumkatakata viungo wakati hupo hai. Shahidi wa hili ni Mboneka Fisimaji, mpwa wa Patauli ambaye yeye alichukuliwa kwa ajili ya kubeba furushi la maiti. Hakuna yeyote aliyejua hili. Kila mmoja, ndugu jamaa na marafiki walijua Charton yupo kikazi Dodoma."

Alichokuwa akikisikia Inspekta Frank kutoka kwa Eddy ni kama muvi anazoziona kwenye televisheni, lakini leo anaona na kusikia kisa hiki laivu kimetokea bongo.


"Kwa kukukumbusha tu afande ni kwamba kule Mwanza alikokaa Charton alimtafuta mtu mmoja na mpenzi wake kabla hajasafiri, akawapeleka kwenye hoteli moja maarufu, akawalipa na pesa, mwanaume akatumia jina lake na kukaa na mwanamke huyo kwa siku mbili.

Lengo ni kama kutakuwa na kusaka ushahidi basi ionekane alikuwa jijini Mwanza kwa siku mbili, hivyo wakati mkewe anapotea na maiti yake kugunduliwa kwenye kiroba alikuwa jijini Mwanza.

Kusema kweli huyu jamaa ni mzuri sana kwenye kuficha ushahidi. Bahati mbaya tu amekutana na mimi, vinginevyo..."

"Haikuwa mchezo Eddy." Akadakia Inspekta Frank.

"Ni kweli yalikuwa ni mauaji yaliyopangwa taratibu na kifundi sana. Fikiria hadi leo Charton yupo uraiani, hakuna ndugu, jamaa au fununu tu zinazoonyesha kuwa amehusika katika tukio la kumuua mkewe. Namsifu amelifanya kwa ufundi wa hali ya juu. Alipomaliza unyama huo na mwenzake Patauli, walivirundika viungo kwenye kiroba, halafu wakafunga vizuri kwenye boksi, wakambebesha yule jamaa ambaye nimesema atakapokamatwa Charton na hawara yake Rukia aachiwe huru, wakaondoka na maiti kutoka Banana kwa Mapunda hadi kituoni, wakakodisha taxi ya dereva mmoja anayepaki pale Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Dar es Salaam aliyewapeleka hadi Magomeni Mikumi. Safari ya dereva yule na Mboneka iliishia pale, wakabaki wauaji wenyewe. Lengo ilikuwa ni kuwapoteza maboya wasijue kinachoendelea. Na mpaka wanabeba boksi hilo la maiti, dereva na Mboneka walikuwa hawajui kuna nini zaidi ya mzigo tu wa biashara. Lakini wakati nikimhoji Mboneka aliniambia alishuhudia mateso na Tessy mbele ya mumewe na mjomba wake Patauli, lakini hakuhisi kama mzigo alioubeba ni wa maiti."




**"Ilikuwaje unakahisi kuwa mumewe anaweza kuhusika na hilo wakati siku ya kuuawa ilionekana hayupo Dar, bali Dodoma kikazi?" Afande Frank akamuuliza.**

Afande Frank alikuwa anamtazama Eddy kama vile mtu anayemtazama binadamu wa maajabu ambaye ameletwa duniani kufumbua mambo ambayo kwa macho ya uchunguzi wa kibinadamu wa kawaida ulikuwa umeshindikana.

"Baada ya kuachana nao Magomeni Mikumi, wakakodisha gari lingine hadi Kinondoni Biafra. Pale waliushusha mzigo na waliwaita wale jamaa wanaobeba takataka na masela, wakawalipa pesa nyingi kidogo ili wakautupe.

Waliwadanganya kuwa ni takataka. Lakini kwa jinsi walivyoufunga wale jamaa waliona kama vile mbali na takataka lakini kuna mali. Wakaelekea chimbo ili kuona kuna nini, walipofungua wakakutana na viungo vya mwili wa binadamu. Waliogopa na wakaona wasipofanya akili wanaweza kukamatwa na ushahidi. Walichoamua ni kushuka chini maeneo ya Kinondoni Msisiri wakiwa na mzigo huo wakati huo boksi walikuwa wameshalifungua, mwili wa marehemu ulikuwa kwenye kiroba, wakautupa upenuni mwa moja ya nyuma za wakazi wa hapo."

"Ilikuwa ni nyumba ya bibi mmoja anaitwa Bi Mkali, nakumbuka pale nilimtuma Sajenti Moses kwenda kumuhoji yule bibi na Koplo Ben naye nikampaka kazi ya kwenda kuhoji kwingine, kumbe muuaji anatoka mbali na kabisa na ni mtu ambaye huwezi kumtarajia." Akashangaa Inspekta Frank.

"Ni kweli, si huyo bibi, wapangaji wake, wala wajirani waliojua chochote. Mauaji yalifanyika Ukonga, maiti ikatupwa Kinondoni Msisiri, na mabaki ya mwili ya Tessy yalivumbuliwa na mbwa baada ya kusikia harufu. Nina uhakika kuwa wauaji walimiminia viungo dawa fulani ya kukausha ili mwili ukae muda mrefu bila kutoa harufu kwa ajili ya usalama wao.

"Kingine ambacho mnapaswa kujua Inspekta Frank ni kwamba mhalifu huwa na akili nyingi sana. Kwa sababu yeye akapanga nini cha kufanya baada ya kutekeleza uhalifu. Kwa maana hiyo si rahisi sana kukuta maiti nje ya nyumba fulani, basi muuaji akawa amelala humo. Huwa nashangaa sana wanavyowekwa ndani watu kuidia polisi kwa sababu tu maiti imekubwa asubuhi nje ya nyumba yao, au duka lao. Hawa anachotakiwa ni kutoa tu ushahidi, au kile ambacho wanakifahamu. Katika ushahidi wao wanaweza kuwafanya muanze kumhisi muuaji. Mara nyingi, maiti inapopatikana, popote pale, ujue muuaji atakuwa kilometa nyingi kutoka hapo. Anaukibia ushahidi. Wale wanaokamatwa au kuwekwa ndani mara nyingi wanaonewa tu. Kwa hali ya kawaida hakuna anayeweza kuua mtu akaendelea kulala ndani humo humo."

"Ilikuwaje unakahisi kuwa mumewe anaweza kuhusika na hilo wakati siku ya kuuawa ilionekana hayupo Dar, bali Dodoma kikazi?" Afande Frank akamuuliza.

"Wapelelezi, katika ile kanuni yetu ya aina ya za mauaji na wauaji, hii ukiitazama imeangukia kwenye kundi la nne na tano, kwa hiyo nilianzia hapo. Inasema hivi.

Kundi la nne kuja jamaa wanaitwa 'cold blood killers'. Hawa ni watu wa kuogopwa mno kama ukoma. Ni kama vile hawana roho wala hisia. Ni kama hawakuzaliwa binadamu ila ni wanyama waliojivika ngozi ya binadamu. Wakati mwingine unaweza kusema wana matatizo ya akili. Wao huua taratibu na kwa mateso makubwa mno. Hawa ndiyo wale watu ambao utasikia wamemuua mtu na kuwatenganisha viungo kimoja baada ya kingine. Anaweza kuua kwa leo kukukata kidole, mkono, mguu, kila siku kimoja kimoja hadi mhusika atakapokufa kifo cha mateso. Wapo wanaokwenda mbali zaidi, wanaweza kujirekodi na hata wakati mwingine kupika viungo.

Namba tano ni wauaji kwenye msongo wa mawazo 'stress,' au maumivu ya mapenzi. Wauaji hawa hufikia kuona kila mmoja ni adui yake. Anaweza kuchukua silaha na kwenda hadi kwenye kadamnasi ya watu na kuwafyatulia risasi kwa raha zake. Na mara nyingi watu hawa na wao kuishia kujimaliza wao wenyewe watakapobakisha risasi ya mwisho kwenye bastola.

Mauaji ya Tessy yanaingia kwenye aina hizo mbili namba nne na tano, hakuna mtu anayetenganisha kiungo cha mtu kwa kutaka tu kuiba au kuchukua pesa. Ni lazima mauaji alikuwa na hasira kali, ama ni mtu ya aliyedhulumiwa, au wivu mkali ya kimapenzi. Kwa maana hiyo nilimtafuta kwanza mjomba wa marehemu, akanipa majina ya watu ambao niliona nianze nao upelelezi, mmoja wapo ni mume wa marehemu Charton."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# NEW CITY FC YATAMBA KUISIMAMISHA KMKM

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

TIMU ya New City FC imesema inahitaji kupata ushindi katika mechi yake ya Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya mabingwa watetezi, KMKM itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Mau A.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Razak Salum alisema amekiandaa vyema kikosi chake ili kukabiliana na wakongwe hao ingawa anafahamu mechi hiyo itakuwa ngumu.

Salum alisema baadhi ya vitu alivyofanyia kazi katika kikosi chake ni kuwaondoa hofu wachezaji wao na kuwasisitiza kucheza kwa kujiamini ili wafikie malengo yao.

Kocha huyo alisema kikosi chake pia kina uzoefu katika ligi hiyo lakini kupoteza kwao michezo miwili mfululizo iliyopita kumewapa hasira ya kuhakikisha wanapata alama tatu katika mchezo wa leo.

"Sote tunaijua KMKM ni miongoni mwa timu iliyochukua mataji mengi katika Ligi Kuu Zanzibar, lakini pia ina wachezaji wazuri na wazoefu, hivyo lazima twende na mbinu ambayo hatutapoteza mchezo huo," alisema kocha huyo.

Aliongeza anaamini wakipata ushindi katika mechi hiyo watapanda katika msimamo wa ligi na hivyo kuanza kuondoka mkiani.

New City FC yenye pointi tano inashuka dimbani leo ikiwa katika nafasi ya 13 kwenye msimamo wa ligi hiyo baada ya kushinda mchezo mmoja, sare mara mbili na imepoteza michezo mitatu wakati wapinzani wao KMKM wakiwa nafasi ya saba na pointi 10 mkononi.

Ligi Kuu Zanzibar inayoshirikisha timu 16 ndio hutoa mwakilishi wa visiwa hivyo katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Bingwa wa michuano ya Kombe la FA Zanzibar yeye hupata nafasi ya kushiriki mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Mzunguko wa saba wa ligi hiyo ulitarajiwa kuendelea tena jana jioni kwa Mlandege kuwakabili Maafande wa Kipanga FC.




Rais wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), Gianni Infantino (katikati), akiwa na viongozi kutoka nchi mbalimbali ambao wamekuja Tanzania kushuhudia mechi ya ufunguzi ya African Football League kati ya Simba na Al Ahly iliyochezwa jana jioni. **PICHA: TFF**

## Maguri kuikosa Dodoma Jiji FC

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Geita Gold inatarajia kuivaa Dodoma Jiji katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Nyankumbu, Geita bila straika wake tegemeo, Elius Maguri.

Straika huyo nyota aliumia katika mechi dhidi ya Yanga iliyochezwa Oktoba 7, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.

Daktari wa Geita Gold, Abdallah Chuma alisema wachezaji wengine wa timu hiyo wako fiti na wanausubiri kwa hamu mchezo huo wa nyumbani.

"Maguri hayupo mjini Geita, ameondoka kwenda kupata matibabu zaidi. Ana maumivu ya kifundo cha mguu wa kushoto jambo limemfanya asifanye hata mazoezi na timu hiyo mpaka sasa, kama unakumbuka alipata majeraha kwenye mechi dhidi ya Yanga," alisema Chuma.

Maguri aliumia baada ya kugongana na beki wa Yanga, Bakari Mwamnyeto na alishindwa kuendelea na mchezo, badala yake akaingia Velentino Mashaka, mechi ambayo iliisha kwa Geita Gold kupigwa mabao 3-0.

Kocha wa magolikipa wa Geita Gold, Augustine Malindi amesema baada ya kupoteza mechi mbili zilizopita hawataki kuona wanafungwa tena wakiwa nyumbani.

"Najua tumepoteza, lakini mechi ambazo tulizopoteza ni ngumu, KMC ni wazuri na Yanga ni timu kubwa ngumu, tulicheza vizuri sana lakini makosa madogo madogo yalitugharimu, tunaahidi kwenye mechi hii tutakwenda kuwapa furaha mashabiki wetu, wasikate tamaa waje kwa wingi kutushangilia," alisema kocha huyo.

Geita Gold iko katika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi nne baada ya kuishinda mechi moja, sare mbili na kupoteza michezo miwili.

Mechi nyingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo ni kati ya Ihefu dhidi ya Coastal Union wakati Singida Fountain Gate watawakabili wenyeji wao Namungo kwenye Uwanja wa CCM Liti uliopo mkoani Singida.

# *Yanga kumchangia faini Kamwe*

**Na Adam Fungamwango**

BAADHI ya wanachama na mashabiki wa Yanga wameanzisha mchango kwa ajili ya kumlipia faini Ofisa Habari wa timu hiyo, Ali Kamwe ambaye ametozwa Sh. milioni moja kwa kosa la kumdhalilisha mwamuzi, Tatu Malogo, imefahamika.

Kamwe alitoa kauli ya kumdhalilisha Malogo baada ya kumaliza kuchezesha mechi ya Ligi Kuu Bara kati ya Singida Fountain Gate dhidi ya Simba.

Adhabu hiyo imetolewa na Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB).

Kamati hiyo pia imewasimamisha waamuzi wasaidizi wawili, Nestory Livangala kutoka Iringa na Abdallah Bakenga wa Kigoma kutoka na kushindwa kumudu majukumu yao.

Pia Yanga imetozwa faini ya Sh. milioni mbili kwa makosa tofauti, yote yakifanyika kwenye mechi moja tu dhidi ya Ihefu iliyochezwa Oktoba 4, mwaka huu kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbarali, Mbeya, wenyeji wakitoka na ushindi wa mabao 2-1.

Mwamuzi msaidizi namba mbili katika mechi kati ya Prisons dhidi ya Simba iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine, jijini Mbeya, Livangala ameondolewa kwenye ratiba kwa mizunguko mitano kwa kosa la kushindwa kutafsiri vyema sheria za mpira wa miguu.

Yanga pia imetozwa faini wa Sh. milioni moja kwa kosa la mashabiki wake kurusha chupa za maji uwanjani baada ya Ihefu kufunga bao la pili huku ikitozwa kiasi kama hicho kwa sababu ya maofisa wake kuonekana wakipinga maamuzi ya waamuzi wa mchezo dhidi ya Ihefu.



## ZISIKUPITE

### MOURINHO ATAJWA MADRID

KOCHA AS Roma, Jose Mourinho yuko tayari kurejea Real Madrid msimu huu, akichukua nafasi ya kocha wa sasa wa Los Blancos, Carlo Ancelotti ambaye anatarajiwa kuelekea Brazil. (***Mundo Deportivo***)

### SANCHO MAMBO MAGUMU

WINGA wa Manchester United, Jadon Sancho hatachezeshwa hadi amwombe radhi Kocha, Erik ten Hag. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 aliachwa nje wakati United ikicheza dhidi ya Arsenal mwezi uliopita kwa sababu ya kutokidhi viwango vya mazoezi. (***Guardian***)

### MUSIALA NJIA PANDA

LIVERPOOL inaogopa kumnunua kiungo wa kati, Jamal Musiala mwenye umri wa miaka 20 ingawa mchezaji huyo hana furaha kwa kutokana na kukosa uhakika wa namba katika kikosi cha kwanza cha Bayern Munich. (***Mirror***)

### HOWE AIKATAA ENGLAND

KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe hataki kuwa kocha ajaye wa England licha ya FA kumjumuisha kwenye orodha fupi ya watu wanaotarajiwa kuchukua nafasi ya Gareth Southgate. (***Telegraph***)

### CHELSEA KUMBANA MAATSEN

CHELSEA inatazamiwa kutekeleza chaguo la kuongeza mkataba wa Ian Maatsen mwenye umri wa miaka 21, hadi majira ya joto ifikapo mwaka 2025 huku The Blues wakitumaini watafanikiwa kumzuia beki huyo kujiunga na Barcelona. (***Evening Standard***)

### SUAREZ ANUKIA MIAMI

KOCHA Mkuu wa Inter Miami, Gerardo Martino amethibitisha timu yake ina nia ya kumnunua mshambuliaji wa Uruguay, Luis Suarez na anatumaini kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, ambaye kwa sasa anachezea Gremio ya Brazil. (***ESPN***)

### LAPORTA AMKATAA MESSI

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta amekataa kumsajili, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 36 kutoka Inter Miami ifikapo Januari, baada ya kujaribu kumrejesha nyota huyo wa Argentina huyo Camp Nou msimu uliopita. (***Fabrizio Romano***)

### DECO : MESSI ATARUDI

MKURUGENZI wa Michezo wa Barcelona, Deco bado anasisitiza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi atarejea katika klabu yake ya zamani. (***Sun***)


### LINGARD KUTUA AL ETTIFAQ

KLABU ya Al Ettifaq ya Saudi Arabia iko tayari kumsajili mchezaji huru, Jesse Lingard. Kiungo huyo wa zamani wa Manchester United mwenye umri wa miaka 30, ambaye anafanya mazoezi na kikosi cha Steven Gerrard, amekuwa bila klabu tangu alipoondoka Nottingham Forest msimu huu. (***ESPN***)

### WAN-BISSAKA, LINDELOF SAFI

KLABU ya Manchester United itaongeza mkataba wa mwaka mmoja kwa mabeki Aaron Wan-Bissaka na Victor Lindelof na kusaini mkataba mpya na kiungo Hannibal Mejbri. (***Manchester Evening News***)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CASEMIRO KUIKOSA SHEFFIELD UNITED

**SAO PAULO,** Brazil

**●●● Ni kutokana na jeraha alilopata alipokuwa akiitumikia Brazil...**

CASEMIRO ataukosa mchezo wa Ligi Kuu England wakati Manchester United itakapoivaa Sheffield United leo baada ya kushauriwa na klabu hiyo kubakia Brazil ili kuendelea kupata nafuu kutokana na tatizo la kifundo cha mguu.

Kiungo huyo wa kati alipata jeraha hilo wakati Brazil ilipotoka sare ya 1-1 na Venezuela lakini akatangazwa kuwa fiti vya kutosha kucheza dakika 90 katika kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Uruguay Jumanne iliyopita.

**Casemiro alitarajiwa kurejea United juzi, lakini alishauriwa na klabu hiyo kusalia Brazil ili kumsaidia kupona.**

Anatazamiwa kurejea Carrington mapema wiki ijayo, ingawa pia atakosa mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya FC Copenhagen itakayofanyika Jumanne kwenye Uwanja wa Old Trafford kutokana na kufungiwa baada ya kadi nyekundu katika mechi waliyochapwa mabao 3-2 na Galatasaray.

United wameelezea jeraha la mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 kama "suala dogo" na kuna matumaini atakuwa fiti kwa ajili ya dabi ya Manchester itakayochezwa kwenye Uwanja wa Old Trafford Oktoba 29, mwaka huu.

Kocha, Erik ten Hag ana matumaini ya kumtumia beki wa kushoto, Sergio Reguilón kwa ajili ya safari ya kwenda Sheffield United baada ya raia huyo wa Hispania kukosa mechi nne zilizopita kutokana na tatizo la misuli ya paja.

Reguilon anayecheza kwa mkopo kutoka Tottenham Hotspur na alifanya mazoezi na kikosi huko Carrington Alhamisi pamoja na Sofyan Amrabat, ambaye alikosa mechi za Morocco dhidi ya Liberia na Ivory Coast wakati wa mapumziko ya kimataifa.

Raphaël Varane bado hana shaka baada ya kukosa ushindi wa United dhidi ya Brentford.

Majeruhi wa muda mrefu Lisandro Martínez, Luke Shaw na Tyrell Malacia bado hawajawa fiti huku Jadon Sancho akiendelea na programu ya mazoezi binafsi.

# Suarez awaniwa Inter Miami

**MIAMI,** Marekani

KOCHA Inter Miami CF, Gerardo "Tata" Martino amethibitisha klabu yake kuendelea kutaka kumsajili mshambuliaji mkongwe, Luis Suárezi.

Akizungumza na vyombo vya habari siku moja kabla ya mchezo wa mwisho wa nyumbani wa Miami wa msimu, Martino alisema wanaendelea kutathmini uwezekano wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 kutoka Uruguay.

"Katika uchambuzi wetu wa msimu ujao, na mahitaji ambayo tunaweza kuwa nayo, tuna uchambuzi na tunamhitaji Suarez," alisema Martino.

"Wakati ukifika wa kufanya hali ya Suárez kuhusiana na Inter Miami rasmi, tutakuwa tayari kwenda katika mwelekeo unaolingana."

Kama ilivyothibitishwa mapema mwezi huu na kocha wake wa sasa wa Grêmio, Renato Gaucho, Suárez ataondoka katika klabu hiyo yenye maskani yake Porto Alegre mwishoni mwa msimu wa Serie A ya Brazil Desemba, licha ya kuwa katika nusu tu ya mkataba wake wa miaka miwili.

"Alikuwa mtu aliyepitia hapa na sio tu alijidhihirisha huko Grêmio, lakini ninaamini Brazil yote inaitambua," alisema Gaucho. "Nimekuwa na furaha kufanya kazi naye. Tutamkumbuka sana."

Suárez mfungaji bora wa muda wote wa Uruguay akiwa na mabao 68 katika mechi 137 alizocheza na La Celeste, kwa sasa ndiye mfungaji bora wa Grêmio msimu huu akiwa na mabao tisa katika michezo 27 ya ligi.




# RAMSDALE: NINAUMIA SANA KUPOTEZA NAMBA

**LONDON,** England

GOLIKIPA Aaron Ramsdale alisema "nateseka na kuumia" baada ya kupoteza nafasi katika kikosi cha kwanza cha Arsenal kwa David Raya, lakini akasisitiza yeye na mwenzake wako kwenye mahusiano mazuri.

Ramsdale alikuwa chaguo la kwanza tangu ajiunge na timu hiyo mwaka 2021 na alicheza mechi zote 38 za Ligi Kuu England msimu uliopita, lakini aliwekwa benchi kwenye mechi nne za mwisho za ligi ya timu hiyo ya London Kaskazini huku Raya, ambaye aliwasili kwa mkopo kutoka Brentford Agosti mwaka huu akichukua nafasi yake.

"Nadhani kwa sababu ni mara ya kwanza kutokea na hali imekuwa ngumu," alisema Ramsdale akiwaambia waandishi wa habari.

"Ikiwa ni mimi au David ambaye anacheza tunahitaji kuwa na uwezo wa kuzingatia tu na kucheza. Tunapaswa kukabiliana nayo na ndivyo tunafanya. Tunafanya kazi pamoja kitaaluma vizuri sana.

Ramsdale aliitwa kwenye kikosi cha Kocha, Gareth Southgate cha England kwa mechi ya kirafiki mwezi huu dhidi ya Australia na kufuzu euro 2024 dhidi ya Italia, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 hakucheza katika mechi zote mbili.

"Kwangu mimi nahitaji kurejea katika timu yangu ili kuendelea kuchaguliwa kwa ajili ya England na kuendelea kuumiza kichwa kwa kocha kwa sababu kama sichezi, basi huo ni uamuzi rahisi kwake," aliongeza Ramsdale.

"Ni wasiwasi, ni mara ya kwanza kujikuta katika hali hii."

Arsenal, ambao wanashika nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu England watasafiri kumenyana na Chelsea hapo leo.



# Kudus alikaribia kutua Chelsea

**LONDON,** England

CHELSEA ilifikia makubaliano ya binafsi na Mohammed Kudus kabla ya uhamisho wake wa pauni milioni 38 kwenda West Ham majira ya joto, na hiyo ni kutokana na ofa ndogo iliyotolewa kwa Ajax, wakala wa mchezaji huyo amethibitisha.

The Blues ilianza msimu mwingine wa matumizi makubwa ya fedha kwenye uhamisho, kwa kutumia kiasi kikubwa cha fedha kwa Moises Caicedo, Romeo Lavia, Nicolas Jackson, Christopher Nkunku, Axel Disasi na Cole Palmer.

Kudus alikuwa akivutiwa na Manchester United, baada ya kufanya kazi na Erik ten Hag kule Ajax, na Arsenal, lakini, Chelsea walikuwa wa kwanza kufanya mazungumzo na kambi ya mchezaji huyo.

Katika mwonekano wake kwenye kituo cha redio cha RMC, wakala, Jen Mendelewitsch alizungumzia nia ya Chelsea kwa mteja wake, na kusema mambo yaliharibika dakika za mwisho kwa Ajax kukataa ofa iliyowekwa mezani.

"Chelsea ilikubaliana maslahi binafsi na Kudus," alieleza, kabla pia kufichua The Blues "walipunguza ofa" kwa Ajax kuwa pauni milioni 17.5.

Kulikuwa na kidokezo cha juhudi za muda mrefu za kujaribu kumsajili Caicedo, ambazo Chelsea ilifanya kwa pauni milioni 115, zilikuwa ngumu sana.

"Ukweli Chelsea walichukuliwa kabisa na uhamisho wa Caicedo, ambao ulichukua nguvu zao zote," aisema Mendelewitsch.

Kudus alijiunga na Ajax kutoka Nordsjaelland ya Denmark mwaka 2020 muda mfupi kabla ya kufikisha umri wa miaka 20, ingawa haikuwa hadi msimu uliopita ambapo alijiunga na klabu hiyo ya Amsterdam na kujitangaza.

Alifunga mabao 18 katika mashindano yote wakati wa msimu huo, ikiwa ni pamoja na manne katika Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Tangu atue West Ham, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, amefunga mara mbili katika mechi nane kwenye michuano yote, lakini bado hajaanza mechi ya Ligi Kuu England.



HABARI MICHEZO

# SIMBA, MAZEMBE RASMI KUSHIRIKIANA

Na Somoe Ng'itu

RAIS wa TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Moise Katumbi amesema klabu yake imefikia makubaliano rasmi ya kushirikiana katika masuala mbalimbali na vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba.

Katumbi alisema hayo baada ya kumaliza kikao na mabosi wa Simba na baadaye kwenda kushuhudia mazoezi ya mwisho ya kikosi cha Wekundu wa Msimbazi kilichokutana na mabingwa wa Afrika, Al Ahly kutoka Misri.

Akizungumza na Nipashe, Katumbi alisema anaamini ushirikiano wa klabu hizo mbili utasaidia kuzipa mafanikio na hatimaye kufanya vyema katika mashindano mbalimbali ya kimataifa wanayoshiriki.

Katumbi alisema amefurahi kuona Simba imepata nafasi ya kushiriki mashindano ya African Football League kwa sababu kupitia michuano hiyo, klabu pamoja na wachezaji watapata nafasi ya kujitangaza kwa timu nyingine za Ulaya.

"Ninawapongeza sana viongozi wa Simba kwa hatua ambayo wamefika, kuongoza klabu ya soka si jambo dogo, kupata mafanikio katika mashindano ya CAF kunatokana na juhudi na jitihada za viongozi na wachezaji.

Mazembe kushirikiana na Simba haijaanza sasa, tulianza huko nyuma tulipomchukua Mbwana Ali (Samatta), tukampata pia Ulimwengu (Thomas), tunaishukuru pia Serikali ya Tanzania kwa kutupokea," alisema Katumbi.

Kuhusu nafasi ya Simba katika michuano ya African Football League, Katumbi alisema mafanikio ya klabu ndio yamewafikisha katika ngazi hiyo na heshima waliyopata ya kucheza mechi ya ufunguzi ni ishara soka la Tanzania limepanda.

"Haya mashindano yataleta mambo mazuri, yataleta fedha nyingi katika timu zetu, imepanza na Simba, Mamelodi na TP Mazembe kwa upande wa SADC, itafungua fursa mbalimbali, niseme tu Simba imestahili kufika hapa ilipo, " alisema Katumbi.


Mmiliki huyo wa mabingwa hao wa zamani wa Afrika aliwataka mashabiki wote wa soka nchini kuwashangilia Simba katika michuano hiyo.

"Kesho (jana), nitakuwa upande wa Simba, hakuna Mazembe, hakuna Yanga, mimi pia nitaiombea Simba ifanye vizuri katika mechi yao," Katumbi aliongeza.

Bosi huyo alisema pia amefurahi kuona Simba imekubali kuwasaidia katika maandalizi ya mechi zao watakazochezea kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na kuahidi ushirikiano huo utazaa matunda kwa klabu zote mbili.

Kwa sasa Simba ina mchezaji mmoja iliyemsajili wa mkopo akitokea TP Mazembe ambaye ni mshambuliaji, Jean Baleke.

TP Mazembe inatarajia kucheza mechi yake ya michuano ya AFL kesho dhidi ya Esperance de Tunis kutoka Tunisia kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Rais wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Patrice Motsepe kuhusu uwenyeji wa Tanzania katika Fainali za AFCON za mwaka 2027 walipokutana Ikulu jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Mtibwa Sugar hali mbaya

Na Adam Fungamwango

PAMOJA na kumtimua kocha wao Habib Kondo, bado haikuwa dawa kwa Mtibwa Sugar, ikijikuta ikipoteza mechi yake ya nne kati ya sita ilizocheza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na kuendelea kuwa kwenye hali mbaya katika msimamo wa ligi hiyo.

Mtibwa juzi ikiwa nyumbani, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro ilipokea kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Kagera Sugar, ikiwa ni mechi ya tatu kupoteza kwenye uwanja wake wa nyumbani.

Wiki hii, timu hiyo ilimfurusha kocha wake Kondo kutokana na matokeo mabaya na inaelezwa aliyekuwa kocha wa Ihefu, Zubari Katwila anapigiwa upatu kwenda kuchukua mikoa ya Kondo.

Mabao ya Kagera Sugar juzi yaliwekwa wavuni na Ally Nassor dakika ya 30 na Said Omari dakika ya 90, ushindi ambao umeinyanyua hadi nafasi ya sita ya msimamo ikiwa na pointi nane, kabla ya mechi zingine kuchezwa jana huku Mtibwa Sugar ikizidi kuporomoka.

Huo ulikuwa ushindi wa pili kwa Kagera Sugar ambayo kabla ya mechi hiyo ilikuwa imeshinda mechi moja tu dhidi ya Geita Gold.

Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Macky Mexime amesema wamepata ushindi kutokana na kutumia vyema nafasi.

"Mechi ilikuwa nzuri wao walishambulia mara nyingi zaidi kuliko sisi, nafikiri sisi tulichofanikiwa ni kutumia nafasi tulizozitengeneza tofauti na wao, wangekuwa makini dakika 15 za mwanzo ilikuwa watuadhibu hata mabao matatu," alisema.

Kaimu Kocha Mkuu wa Mtibwa Awadh Juma amesema bado anaendelea kupambana kurekebisha makosa ndani ya kikosi chake.

Kipigo hicho kinaishusha Mtibwa hadi mkiani, ikichukua nafasi ya Coastal Union ambayo wanazidiana mabao ya kufungwa.

## Gamondi aandaa...

INATOKA UK 24

wafunga katika Ngao ya Jamii, nimekisuka vyema kikosi changu na kila mchezaji anatambua jukumu lake. Hatutakuwa tayari kupoteza mechi ya pili katika ligi, tumeona ubora wa Azam, lakini pia wanamapungufu na tutatumia kwa ajili ya kusaka ushindi mapema na kutowapa nafasi ya kuleta madhara kwetu," alisema Gamondi.

Alisema anatambua Azam FC inawachezaji wazuri na wataingia uwanjani kwa ajili kulipa kisasi, lakini wamejipanga kuwakabili na wanahitaji ushindi katika mchezo huo muhimu wa Ligi Kuu.

"Tupo katika mbio za ubingwa, hatuwezi kukubali kupoteza mchezo huu, tunahitaji ushindi kuhakikisha tunajiweka katika mazingira mazuri ya mipango yetu katika ligi hii," alisema Kocha huyo.

Mara ya mwisho Yanga kufungwa na Azam ilikuwa Aprili 25, 2021, katika mchezo Ligi Kuu msimu wa 2020/21, ambapo Azam ilishinda bao 1-0 kwa bao la Prince Dube.

Baada ya hapo timu hizo zimecheza mechi sita, Yanga ikishinda nne na kutoka sare mechi mbili, kati ya mechi hizo mechi tano za Ligi Kuu na moja ya Kombe la FA.

# *Historia yaandikwa Tanzania*

INATOKA UK 24

45 lililotokana na makosa ya safu ya ulinzi ya Simba walioshindwa kukaba na kutegeana na kumfanya Slim kupachika bao hilo baada ya kazi nzuri iliyofanywa na Kahraba ambaye alitoa pasi ya 'upendo' kwa mfungaji ambaye alimchambua kipa wa Simba, Salim.

Mpaka kipindi cha kwanza kinamalizika, Al Ahly ambao ni mabingwa wa Afrika walikuwa mbele kwa bao 1-0

Kipindi cha pili kilianza kwa kasi huku Simba wakionekana kubadilika zaidi na kucheza soka la la kasi na iliwachukua dakika nane tu kabla ya Kibu kusawazisha bao la utangulizi akijitoa muhanga kwa kupiga kichwa cha 'kuchumpa' mbele ya beki wa Al Ahly aliyekuwa anajiandaa kuokoa mpira huo.

Bao hilo lilitokana na kazi kubwa iliyofanywa na Saido Ntibazokiza, Clatous Chama na Jean Baleke aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Miquissone.

Simba iliendela kumiliki mpira kuishambulia Al Ahly na katika dakika ya 60 Kanoute aliipatia bao la pili akiunganisha kwa kichwa mpira wa kona uliyopigwa na Ntibanzokinza.

Wakati mashabiki wa Simba bado wakiwa na furaha, makosa yaliyofanywa na wachezaji wa timu hiyo katika kujipanga kuokoa mpira wa faulo ulimuwezesha Kahraba kuiswazishia timu yake katika dakika ya 63.

Ulikuwa ni mpira wa faulo ambao ulitemwa na kipa Salim, lakini wachezaji wa Simba walizubaa na kumpa nafasi Kahraba kutumbikiza nyavuni.

Licha ya Simba kufanya mabadiliko kwa kuwatoa Kibu, Chama, Kapombe na kuingia Israel Mwenda, John Bocco na Willy Onana bado hawakuweza kubadilisha matokeo hayo licha ya Ntibanzonkiza kukosakosa bao baada ya shuti lake kugonga mwamba katika dakika ta 75.

Nyota wa Al Ahly, Kahraba alijibu shambulizi hilo dakika za mwisho za mchezo hata hivyo mpira wake uligonga mwamba na kuokolewa na wachezaji wa Simba.

Baada ya matokeo hayo Timu hizo sasa zinasubiri kurudiana kwenye mchezo utakaochezwa Jumanne ijayo nchi Misri.

Mshindi wa jumla kwenye mchezo huo atakutana na mshidi kwenye mchezo kati ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini na Atletico Petroleos de Luanda ya Angola kwenye hatua ya nusu fainali.

Wakati huo huo, Rais wa Shirikisho la Mpira wa miguu Barani Afrika (CAF,), Patrice Motsepe, amesema anaamini kuwa mashindano hayo mapya ya Afrika Football League yanaenda kuleta chachu kwenye mpira wa Afrika.

Akizungumza na waandishi wa habari kabla ya ufunguzi wa michuano hiyo jana, alisema anaamini mashindano ya AFL yataenda kuongeza ushindani kwenye mashindano yaliyoandaliwa na CAF lakini pia yataongeza ushindani kwenye fainali za mataifa ya Afrika (AFCON).

"Tunataka kuinua soka la Afrika na kulifanya la kuvutia na kufikia viwango vya juu jambo ambalo ni muhimu kwa soka la Afrika, msimu huu tutakuwa na timu nane lakini katika msimu ujao wa mashindano kutakuwa na timu 24 bora kwenye viwango vya CAF hata wadhamini wamefurahia mashindano haya, tunahitaji pesa ili kuyafanya mashindano haya kuwa bora zaidi," alisema Motsepe.

Alisema kuwa soka la Afrika limekuwa likikua amefurahishwa na mafanikio ya Morocco, ambao walifika nusu fainali ya Kombe la Dunia nchini Ufaransa, lakini kwenye ngazi ya vilabu TP Mazembe iliwahi kufika fainali ya klabu bingwa ya Dunia.

"Mshindano haya ya African Football League ni historia kwa Tanzania kuyazindua ambayo yanaenda kufanyika kwa mara kwanza, leo (jana), nilikuwa na nazungumza na Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu maandalizi ya mashindano ya AFCON, yalikuwa mazungumzo mazuri, anataka kuona mashindano ya AFCON mwaka 2027 kuwa ya kipekee, nimefurahia kazi inayofanywa na Rais wa Shirikisho la soka nchini Tanzania, Wallace Karia hakika ni kazi nzuri anayoifanya," alisema Motsepe.

Michezo
Jumamosi Oktoba 21, 2023
Nipashe



Casemiro kuikosa Sheffield UK. 21



Winga wa Simba, Kibu Denis akitafuta namna ya kuwatoka mabeki wa Al Ahly kwenye mchezo wa kwanza wa michuano ya African Football League uliochezwa jana kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa, timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2 Kibu akifunga bao la kusawazisha. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

## Gamondi aandaa mbinu mpya kuimaliza Azam FC

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi amesema ameandaa mbinu mpya na kuwapa wachezaji wake kwa ajili ya mchezo wao dhidi ya Azam FC ambao anaamini watafanya vizuri.

Yanga na Azam wanatarajia kuumana keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam wanajangwani hao wakiwa wenyeji wa mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema anafahamu ubora wa Azam FC na ameandaa timu yake kwa umakini kwa kila mchezaji kumpa jukumu lake ili kuchochea kupata matokeo mazuri kwenye mchezo huo.

Alisema maandalizi ya mchezo huo walifanya mara baada ya kumalizika kwa mchezo wao na Geita Gold FC , na kikosi chake kipo imara na watahakikisha wanafanikiwa kupata ushindi katika mchezo huo.

"Huu ni mchezo mkubwa sana, Azam FC hawatakubali kupoteza kwa mara nyingine baada ya ku-

INAENDELEA UK 23

# Historia yaandikwa Tanzania

## Ya uzinduzi wa michuano mipya ya AFL, watu maarufu katika soka washuhudia. Simba, Al Ahly haijaisha mpaka iishe...

**Adamu Fungamwango na Saada Akida**

HISTORIA ya soka imeandikwa Tanzania, ndio.., ni ya uzinduzi wa michuano mikubwa Afrika ya African Football League (AFL) huku viongozi wa soka Afrika na watu maarufu katika soka Duniani wakishuhudia tukio hilo kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Miongoni wa watu hao maarufu waliokuwepo uwanjani kushuhudia uzinduzi na mchezo wa ufunguzi ni pamoja na Rais wa Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), Gianni Infantino, Rais wa Shirikisho la Mpira wa miguu Barani Afrika (CAF), Patrice Motsepe, Kocha wa zamani wa klabu ya Arsenal, Arsene Wenger, Mwamuzi maarufu za zamani wa kimataifa wa FIFA kutoka Italia Pierluigi Collina na wengineo.

Uzinduzi huo ulifuatiwa na mchezo wa kwanza wa ufunguzi wa michuano hiyo kati wawakilishi wa kutoka ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, Simba, dhidi ya wenzao kutoka Afrika Kaskazini, Al Ahly ya Misri.

Kabla ya mchezo huo kulikuwa na sherehe za uzinduzi ambapo burudani mbalimbali zilifanyika ikiwa pamoja na msanii maarufu wa Tanzania, Ali Kiba kutumbuiza mbele ya maelfu ya watazamaji waliojitokeza uwanjani hapo.

Baada ya sherehe za uzinduzi ulifuata mchezo uliohusisha miamba hiyo ambapo mabao mawili ya vichwa, yaliyofungwa kipindi cha pili ndani ya dakika saba na Kibu Denis pamoja na Sadio Kanoute yaliirudisha Simba mchezoni kwani mpaka mapumziko tayari ilikuwa imeshatanguliwa kwa bao 1-0.

Hata hivyo bao hilo lilidumu kwa dakika tatu tu, kabla ya Mahmoud Kahraba ambaye aliisumbua mno ngome ya Simba hajasawazisha na kufanya mchezo huo kumalizika kwa sare ya mabao 2-2.

Matokeo hayo yamefanya vita ya timu hizo katika michuano hiyo mipya kubakia kuwa 'hai' na hivyo katika lugha ya mtaani wanasema haijaisha mpaka iihse kwa kuwa bado kuna dakika 90 nyingine zitakazo chezwa nchini Misri.

Hata hivyo, Simba sasa ina kazi ya kwenda kufanya jijini Cairo Jumanne ijayo kama inataka kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Wawakilishi hao kwenye Ukanda wa CECAFA wanatakiwa kupata ushindi, au sare ya juu ya mabao 2-2 ili kusonga mbele katika michuano hiyo.

Mechi ya jana ilianza taratibu na kwa tahadhari kubwa kwa kila timu zikionekana kusomana, lakini walikuwa ni Al Ahly waliowahi kuwasoma wenyeji wao na dakika ya tano tu nusura wapate bao la kuongoza kama Henock Inonga asingeuondoa mpira uliokuwa unaelekea wavuni, baada ya kutokea purukushani kwenye lango iliyotokana na mpira wa kona.

Simba ilijibu mapigo kwa kufanya shambulizi la kushtukiza lakini shuti la mguu wa kushoto lililopigwa na Kibu liliishia kwenye mikono ya kipa, Mohamed El Shenawy.

Kuanzia dakika ya 12, Al Ahly walifunguka na kuanza kutandaza kandanda safi kiasi cha kuwachanganya viungo wa Simba na mabeki wake na haikushangaza kukosa mabao matatu ya wazi.

Alikuwa ni Reda Slim aliyeondoka na mpira kwenye wingi ya kushoto akiwatoka mabeki wa Simba kiasi cha kipa Ally Salim kutoka langoni, naye akashindwa kumzuia, lakini krosi yake ilitolewa nje na Inonga na kupelekea kona ambayo hata hivyo haikuzaa matunda kwa upande wa Al Ahly.

Mchezaji aliyekuwa akipewa nafasi ubwa ya kuisumbua Simba jana, Percy Tau raia wa Afrika Kusini naye alikosa bao la wazi dakika ya 16 baada ya kubaki na kipa Salim lakini aliunyanyua mpira uliopaa juu kidogo ya lango.

Beki wa kushoto wa Simba, Mohamed Hussein alifanikiwa kwa kiasi kikubwa kumdhiti nyota huyo mpaka alipotolewa kipindi cha pili.

Kahraba aliyekuwa nyota upande wa Al Ahly kwenye mechi ya jana, aliingia kwenye orodha ya wachezaji wa Al Ahly waliokosa mabao baada ya ufanya hivyo dakika ya 19.

Kipa Salim alifanya kazi ya ziada alipookoa mpira wa kichwa wa Kahraba akiunganisha faulo iliyopigwa na la Tau, dakika ya 24 ya mchezo.

Angalau kuanzia dakika 25 Simba ilisimbua Al Ahly kwa kugongeana pasi fupi fupi, na kama wachezaji wake wangekuwa makini wangeweza kupata bao dakika ya 26 kufuatia kazi nzuri ya Chama alipowatoka mabeki wa Al Ahly na kupiga shuti dhaifu lililombabatiza kipa, Shenawy na Luis Miquissone alijikunja na kupiga 'tiktak' iliyotoka nje ya kidogo ya lango.

Al Ahly ilifanikiwa kupata bao dakika ya

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042